# Nipashe

Jumamosi Juni 15, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579945

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Polisi atoweka kazini madai kumpa ujauzito mwanafunzi

UKURASA 3




UKURASA 13

# Muhimbili kutoa uvimbe wa kizazi bila upasuaji

UKURASA 2



Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC), Félix Antoine Tshisekedi Tshilombo, akikagua maendeleo ya ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR, alipotembelea sehemu ya mradi huo, eneo la Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Mishahara, madeni yalamba tril. 12/- ndani ya miezi 10

**WAZIRI** Mpango aeleza kuunganishwa LAPF, PSPF, GEPF, PPF kulivyoathiri mikopo ya ndani, bajeti ijayo yapongezwa kila kona...*Endelea ukurasa wa 2 & 3*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**ANUSURIKA KIFO KWENYE UZAZI**
MKAZI wa Kijiji cha Marasibora, Wilaya ya Rorya mkoani Mara, Belinda Nashon (19), amenusurika kifo baada ya kukosa...

**UKURASA WA 7**

**MBARONI TUHUMA MAUAJI KIONGOZI WA CHADEMA**
JESHI la Polisi mkoani Morogoro linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za mauaji ya mkulima na Katibu Mwenezi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema)...


## Aliyedai kuporwa fedha na polisi aitwa Mwanza

UKURASA 3


**MICHEZO** NDUGAI KUONGOZA WABUNGE KUWASHANGILIA STARS AFCON UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Anusurika kifo kwenye uzazi

**Na Ada Ouko,** RORYA

MKAZI wa Kijiji cha Marasibora, Wilaya ya Rorya mkoani Mara, Belinda Nashon (19), amenusurika kifo baada ya kukosa gari la wagonjwa la kumpeleka kituo cha afya kujifungua na kusababisha kujifungulia zahanati, hali iliyomfanya kutoka damu nyingi na kupoteza fahamu.

Ofisa Muuguzi Mkunga wa Zahanati ya Nyanchabakenye wilayani hapa, Nangi Jacob, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo baada ya Belinda kufika katika zahanati hiyo akiwa katika hali ya kuumwa uchungu.

Jacob alisema ilipofika saa 3:30 usiku, hali ilibadilika baada ya Belinda kujisikia kusukuma mtoto na alimsaidia kwa kuzingatia taaluma yake ya uuguzi na mama huyo alifanikiwa kujifungua mtoto wa kiume ambaye alikuwa na afya njema.

"Baada ya kujifungua huyu mama alipatwa na shida ya kutoka damu nyingi sana na kama unavyojua hii ni zahanati na usiku ule nilikuwa peke yangu ilibidi kuomba msaada kwa ndugu wa mama huyo ambaye alichukua simu yangu na kupiga simu Kituo cha Afya Utegi ili walete ambulance (gari la wagonjwa) ambapo nilijibiwa

INAENDELEA UK. 8

# Muhimbili yaanza kuondoa uvimbe bila upasuaji

**Na Beatrice Shayo**

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili (MNH), imeanza kufanya matibabu ya kuondoa uvimbe kwenye kizazi (Uterine fibroids) bila kufanya upasuaji.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Daktari Bingwa wa Radiolojia, Flora Lwakatare, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema MNH kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Yale na vyuo shiriki vya Emory na Dartmouth vya nchini Marekani, ilianzisha programu maalum ya mafunzo ya tiba ya radiolojia tangu mwaka 2008.

"Tumeweza kutibu uvimbe kwenye kizazi kwa mgonjwa mmoja kupitia tiba ya radiolojia kwa kuingiza mpira wenye chembechembe maalum kwenye mishipa ya damu ambazo zinakwenda kuziba mishipa hiyo inayopeleka damu kwenye uvimbe," alisema.

Dk. Lwakatare alisema baada ya mishipa kuziba, uvimbe unakosa damu au chakula chake na kuanza kusinyaa na kufa.

Alisema mama mwenye uvimbe kwenye kizazi hakuna haja ya kumfanyia upasuaji mkubwa.

Dk. Lwakatare alisema tatizo hilo ni kubwa kwa kuwa kati ya wanawake 10 wanaopimwa wanne wanakutwa na ugonjwa huo.

"Hatari kubwa kama una huo uvimbe utakusababishia kutoweza kupata mtoto, kupoteza damu kwa wingi na hata kupata maumivu makubwa. Kinamama wengi wanatembea nao, madhara ya uvimbe unapokua unasababisha kukosa uzazi, lakini kwa tiba hii tunayoitoa utapata mtoto," alisema.

Aidha, alisema wakufunzi wa awamu ya nne tangu ushirikiano huo uanze umehusisha madaktari bingwa, mafundi sanifu radiolojia, wauguzi wa radiolojia kutoka chuo Kikuu cha Emory na Yale Marekani pamoja na hospitali iliyopo Buffalo, New York, wakiongozwa na Dk. Janice Newsome.

Alisema katika awamu hiyo huduma ambazo zimetolewa ni utoaji

INAENDELEA UK. 8




Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akifungua pazia la jiwe la msingi kuzindua Benki ya Mkombozi, Tawi la Dodoma, jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Thomas Enock. **PICHA: OMR**


MARCAS
DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS LTD.

TANGAZO LA MNADA

NDANI YA SIKU 14

MARCAS DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS LTD [illegible] African Banking Corporation Tanzania Limited ("BancABC") [illegible]






| No | Mali | Eneo | Maelezo ya mali | Tarehe/Muda |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| 1. | [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] |
| 2. | [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] |

MASHARTI YA MNADA

1. [illegible]
2. [illegible]
3. [illegible]
4. [illegible]

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na:
Marcas Debt Collectors and Auctioneers Limited
Safari Hotel Building 2nd Floor,
P.O. Box 16823, Arusha Tanzania
Simu No. 0754 268 383, 0713 268 385, 0787 151 550
www.marcasinvestments.com

215277302


# Mishahara, madeni yalamba tril. 12/- ndani ya miezi 10

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imeliambia Bunge kuwa imefanikiwa kukusanya Sh. trilioni 12.9 kutokana na mapato ya kodi katika miezi 10 ya mwaka huu wa fedha kuanzia Julai, mwaka jana hadi Aprili, mwaka huu.

Hata hivyo, katika kipindi hicho cha miezi 10, serikali imetumia Sh. trilioni 12 kulipa mishahara ya watumishi wa umma na deni la serikali.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mipango, alipowasilishwa bungeni jijini Dodoma juzi mapendekezo kuhusu bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Dk. Mpango alisema katika mwaka huu wa fedha, serikali ilitarajia kupata Sh. trilioni 32.48 kutoka katika vyanzo vyote vya ndani na nje.

Alibainisha kuwa hadi kufikia Aprili, mapato ya kodi yalifikia Sh. trilioni 12.9, sawa na asilimia 87.4 ya lengo wakati mapato yasiyo ya kodi yalifikia Sh. trilioni 2.04 (asilimia 122 ya lengo).

Alisema mapato yasiyo ya kodi yalivuka lengo kutokana na kuimarika kwa matumizi ya teknolojia katika ukusanyaji maduhuli kwenye taasisi za serikali.

Alibainisha kuwa katika kipindi hicho, mapato ya halmashauri yalifikia Sh. bilioni 529.25, sawa na asilimia 72 ya lengo wakati misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo ilifikia Sh. trilioni 1.7 (asilimia 86 ya lengo).

Waziri huyo alifafanua kuwa mikopo ya ndani ikijumuisha mikopo ya kulipia dhamana za serikali zilizoiva, ilifikia Sh. trilioni 33 (asilimia 57.4 ya lengo) na mikopo ya masharti kibiashara ya nje ilifikia Sh. bilioni 692.3.

"Kutofikiwa kwa malengo ya mapato ya kodi kulitokana na sababu mbalimbali, zikiwamo ugumu wa kutoza kodi sekta isiyo rasmi na kuendelea kuwapo kwa upotevu wa mapato kunakosababishwa tatizo la magendo hususan kupitia bandari bubu kwenye mwambao mrefu wa Bahari ya Hindi.

"Pia mwamko mdogo wa wananchi kudai risiti za kielektroniki wanapofanya ununuzi au baadhi ya wafanyabishara wasio waaminifu kutotoa risiti wanapofanya mauzo, Dk. Mpango," alisema.

Aliongeza kuwa kutopatikana kwa mikopo ya ndani kama ilivyotarajiwa kumetokana na kupungua kwa washirika katika soko la fedha la ndani hususan mifuko ya hifadhi ya jamii iliyokuwa kwenye mchakato wa kuunganishwa.

Kwa upande wa mikopo ya nje ya kibiashara, Dk. Mpango alisema upungufu uliojitokeza ulitokana na hali ya masoko ya fedha ya kimataifa kubana zaidi hususan kuimarika kwa Dola ya Marekani na riba kubwa za mikopo.

"Hali hii pia ilisababisha majadiliano na taasisi za fedha za kimataifa kuchukua muda mrefu ili kuhakikisha serikali inapata

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA




Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi (katikati), akipokea sehemu ya msaada wa tani 100 za tende kutoka kwa Kaimu Balozi wa Saudi Arabia hapa nchini, Ahmed Swaaleh El Ghamidiy, uliotolewa na taasisi ya misaada ya kibinadamu ya King Salman ya nchini humo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni mwakilishi wa taasisi hiyo, Abdulnasser Alghamdi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Polisi atoweka kazini madai kumpa ujauzito mwanafunzi

**Na Ibrahim Yassin,** MBEYA

ASKARI polisi, Konstabo Daniel Mlanda wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, ametoroka kituo chake cha kazi baada ya kutuhumiwa kumbaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa kidato cha kwanza mwenye umri wa miaka 14.

Mwanafunzi wa kidato cha kwanza (jina na shule vinahifadhiwa) amedai amekuwa akibakwa na askari huyo akiwa katika lindo kwa shinikizo la mama yake mlezi ambaye alikuwa na urafiki na askari huyo.

Said Juma Mohammed, mjomba wa mwanafunzi huyo, alisema juzi kuwa walipoona mwanafunzi huyo anakuwa mvivu wa kwenda shuleni, alianza kufuatilia mwenendo wake na kubaini kuwa na uhusiano na askari huyo.

Alisema baada ya kufuatilia na kumhoji, alikiri kuwa na uhusiano wa kimapenzi na askari huyo na pia alimweleza kuwa ana ujauzito.

Aisha Mohammed mama mzazi wa mwanafunzi huyo, alisema walipopata taarifa za ujauzito wa mwanafunzi huyo, walianza kumhoji na kumtaja askari huyo kuwa ndiye mhusika baada ya kumwingilia kimwili kinguvu pasipo ridhaa yake.

"Mtoto huyu baada ya kuzidi kumhoji, alisema mara ya kwanza aliingiliwa kinguvu na askari huyo na baadaye alimgeuza kama mkewe na kumsababishia ujauzito licha ya kuwa ni mwanafunzi," alisema.

Baada ya taarifa hizo kuvuja, imeelezwa kuwa vikao vya siri vilianza kufanyika ili kuficha tukio hilo licha ya wananchi kutaka hatua za kisheria zichukuliwe.

William Singo, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Bondeni 'A', alipotakiwa kuzungumzia sakata hilo baada ya kudaiwa kuficha siri, alikanusha kuhusika na vikao vinavyodaiwa kufanyika.

Mkurugenzi wa Kituo cha Msaada wa Kisheria Wilaya ya Kyela, Anna Minga. ni miongoni mwa watu walioeleza kukerwa na tukio hilo, ambaye alisema baada ya kupata taarifa, alianza kufuatilia lakini askari huyo alikimbilia kusikojulikana.

Mbali ya tukio hilo, Mlanda pia anahusishwa na tukio lingine la kumpa mimba binti mwingine Prisca Minga (19) na kumzalisha mtoto wa kiume mwenye umri wa miezi mitano.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Sebastian Mbuta, amethibitisha tuhuma dhidi ya askari huyo na kwamba wanalifanyia kazi suala hilo.

# Polisi wamwita aliyewatuhumu

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limemwita mkazi wa Dar es Salaam, Nixon Moshi, ambaye aliwatuhumu askari watatu mkoani humo kuwa walimpora Sh. 1,188,000 akiwa huko kwa ajili ya kuhani msiba.

Juzi, Nipashe iliandika habari ya Moshi ambaye aliandika barua ya wazi kwenda kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, na kutaka ichapishwe gazetini ili kumsaidia arudishiwe fedha zake alizodai walichukua askari hao.

Jana, alipotafutwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Jumanne Muliro, ili kujua nini kinachoendelea kuhusiana na suala hilo, ndipo alipomtaka Moshi aende Mwanza.

"Kwa sababu jalada la kesi limefunguliwa Mwanza anatakiwa aje huku. Tayari Mkuu wa Upelelezi Mkoa Mwanza (RCO ameshapewa maelekezo," alisema Kamanda Muliro.

Baada ya Nipashe kupokea barua ya Moshi, ilimpigia simu ndipo aliposema pamoja na fedha hizo, zipo zingine kiasi cha Sh. 990,000 zilizotokana na matumizi aliyofanya wakati wote akiwa mkoani humo akisubiri uchunguzi.

INAENDELEA UK. 7

# Bajeti yapongezwa kila kona

**Na Gwamaka Alipipi**

SIKU moja baada ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, kuwasilisha bungeni bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, wasomi, wananchi na wachambuzi wa masuala ya kiuchumi na kijamii, wameisifu wakisema ma imegusa jamii kubwa ya Watanzania.

Dk. Mpango juzi aliwasilisha mapendekezo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 yenye thamani ya Sh. trilioni 33.11, huku akitaja vipaumbele vya serikali kuwa ni kuendeleza viwanda na kilimo, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote.

Vingine ni kuendeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu hususan reli, bandari, nishati, barabara, madaraja, na viwanja vya ndege na upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu, ujuzi, chakula na lishe bora, huduma za majisafi na salama.

Mhadhiri kutoka Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Stephen Kirama, alisema ni bajeti yenye mambo mengi na yanayotia matumaini kwenye sekta zote muhimu kama vile kilimo, miundombinu na biashara.

Alisema licha ya bajeti hiyo kugusa sehemu kubwa ya jamii ya Watanzania, haijamgusa mtu mmoja mmoja, akitolea mfano makato ya kodi ya mshahara (PAYE) ambayo hayajafanyiwa marekebisho.

"Bajeti imegusa sekta za ujumla, kodi za biashara kwani wafanyabiashara wameshushiwa neema, lakini PAYE ambayo inagusa idadi kubwa ya wananchi nayo ingepewa kipaumbele," alisema.

Profesa Haji Semboja wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), alisema ni bajeti nzuri iliyojaa matumaini kwa Watanzania wengi.

Prof. Semboja alisema

INAENDELEA UK. 8



# Aliyehukumiwa kunyongwa aomba kuachiwa

**Na Hellen Mwango**

ALIYEKUWA Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Kinondoni, (kwa sasa mkoa wa kipolisi Kinondoni), Mrakibu wa Polisi (SP) Christopher Bageni, aliyehukumiwa kunyongwa hadi kufa, ameiomba mahakama kumwachia huru kwa sababu uamuzi wa Mahakama ya Rufani Tanzania uliomtia hatiani haukumpa nafasi ya kujitetea.

Kadhalika, amedai kuwa uamuzi wa rufani iliyomtia hatiani iliyofunguliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ulikuwa na hoja za kisheria na kwamba hakupata nafasi ya kujibu na kujitetea.

Madai hayo yalitolewa jana na wakili wa mlalamikaji, Gaudiosis Ishengoma, wakati akiwasilisha hoja za mapitio mbele ya jopo la majaji watatu, likiongozwa na Jaji Stella Mugasha. Majaji wengine ni Ferdinand Wambari na Rehema Kerefu.

Ishengoma alidai kuwa maombi ya mlalamikaji dhidi ya DPP ni kuiomba mahakama kufanya mapitio ya uamuzi wake wa Septemba 16, 2016 uliomtia hatiani mteja wake.

Aidha, alidai kuwa uamuzi huo ulikuwa unalenga kutengua hukumu ya Mahakama Kuu iliyowaachia huru baada ya ushahidi wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha tuhuma za mauaji ya wafanyabiashara watatu na dereva teksi mmoja.

Alidai kuwa pamoja na mambo mengine mamlaka ya mahakama hiyo ni kufanya mapitio uamuzi wake pale inapotokea ukiukwaji wa haki haiwezi kuachwa ikawa hivyo.

"Kwa uhalisia wa kesi hii rufani iliyoletwa na DPP, mlalamikaji hakupata nafasi ya kusikilizwa wakati Mahakama ya Rufani ilipotengua uamuzi wa kumtia hatiani, uamuzi huo wa Mahakama Kuu katika kutafsiri kifungu cha kanuni ya 22 na cha 23 ya adhabu kwamba huwezi kumtia hatiani mtu aliyesaidia kuua ukamwacha aliyeua," alidai na kuongeza.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano kati ya jopo na wakili wa mlalamikaji:

Jaji Wambari: Nini jukumu la Mahakama ya Rufani kusikiliza rufani?

Wakili: Mahakama ya Rufani ina kazi ya kupitia ushahidi kuona kama mahakama ya chini ilikwenda sawa katika kutoa hukumu yake.

Jaji Wambari: Tusaidie mahakama ilisikiliza rufani na kuacha nini?

Wakili: Kuhusu kifungu cha 22 na 23 si sehemu ya hukumu. Watukufu majaji, hukumu ya mahakama kuu ilisema hakuna ushahidi kama watuhumiwa (mlalamikaji na wenzake ambao hawapo mahakamani), katika uamuzi wa rufani ya DPP Bageni

INAENDELEA UK. 8



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akizungumza na wadau waliojitolea kutoa damu wakati wa maadhimisho Siku ya Wachangia Damu Duniani, ambayo kitaifa ilifanyika katika Uwanja wa Furahisha, jijini Mwanza. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Vigogo wadaiwa kufadhili mtandao wa ujangili

**Na Salome Kitomari**

MKURUGENZI wa Kuzuia Ujangili nchini, Robert Mande, amesema baadhi ya viongozi wa serikali, taasisi za umma na binafsi wanafadhili mtandao wa ujangili wa wanyamapori.

Mande, alikuwa kizungumza hivi karibuni na waandishi wa habari 20 wa Tanzania na Thailand walioko kwenye programu ya kuandika habari za kupinga ujangili, iliyowezeshwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania, kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Marekani (USAID).

Alisema biashara ya ujangili ina makosa mengi na hivi karibuni wamebaini makosa yanayofanywa na wataalamu walioko serikalini, mashirika ya umma, mashirika binafsi ambao wamepewa dhamana ya kusimamia rasilimali.

Alisema watu hao huwezesha ujangili kuendelea na kuharibu ushahidi au kesi za ujangili nchini, jambo ambalo lilifanya kazi hiyo kuwa ngumu, lakini kadiri wanavyokamatwa na kufikishwa mahakamani inasaidia.

"Ni biashara ambayo inileta watu wenye uchu wa kutajirika haraka, ni biashara inayoungamisha makosa mengi kama rushwa, utakatishaji wa fedha na ujangili," alifafanua.

"Mtaalamu akijiingiza kwenye rushwa ya kughushi inaitwa "white color crime' tumegundua ndilo tatizo kubwa kuliko lote, ushiriki wa wataalamu maeneo mbalimbali ndiyo unasababisha uhalifu kuendelea na kuwa mgumu kupambana nao," alisema.

Alisema ni rahisi kwa mtu mwenye nafasi kushawishiwa kushiriki kwenye uhalifu bila kujulikana kutokana na nafasi yake.

"Kupambana na mhalifu ambaye humjui na ana nafasi kwenye udhibiti wa sheria ni ngumu sana, tunashirikisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama kwenye kikosi chetu ili tuweze kupambana na watu wote kuanzia ngazi ya chini hadi juu," alisema.

Mande alisema muunganiko wa vyombo hivyo umeleta mafanikio makubwa na ndiyo maana kesi ya 'malkia wa tembo' ilihukumiwa na alifungwa miaka 17 na kulipa faini ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 20.

"Kuanzia mwaka 2016 hadi sasa ujangili wa tembo umeshuka sana, haya ni matunda ya ushirikiano baina ya vyombo vyote vya serikali na sekta binafsi," alibainisha.

Alisema ujangili ulikuwa tishio miaka ya 2000 hadi 2014, asilimia 60 ya tembo walitoweka na ndipo serikali ilianzisha mpango wa kitaifa wa kupambana na ujangili.

Alisema lengo ni kukabiliana na ujangili, biashara haramu ya wanyamapori na mazao ya misitu na ilifanyika operesheni tokomeza kuonyesha ukubwa wa tatizo.

Mande ambaye ni Mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Kuzuia Ujangili nchini, alisema biashara hiyo ilishamiri kutokana na bei kuwa kubwa nchi za Asia kwa kuwa kilo moja iliuzwa Dola 500 ikiwa Tanzania na ikiwa China ni Dola 2,000.

# Samia aonya benki mitandao uhalifu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, imezitaka benki kuepuka kujiingiza katika kashfa na mitandao ya kutakatisha fedha kinyume na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Kifedha na sheria zingine za nchi.

Samia aliyasema hayo jana wakati akifungua tawi la Benki ya Biashara ya Mkombozi jijini Dodoma.

Alisema benki zinapaswa kuwa makini katika kuhakikisha kuwa katika utendaji wa kazi wa kila siku kutojiingiza katika kashfa yoyote ya utakatishaji wa fedha.

Kwa mujibu wa Samia, vitendo hivyo vya utakatishaji fedha vitachangia katika kuharibu sifa ya benki hali ambayo wateja watakosa imani nayo.

Aidha, aliwataka Watanzania kujijengea tabia ya kutumia huduma za kibenki na kuacha kulala na fedha chini ya mito ya vitanda.

"Watanzania lazima tubadilile, tuache kuhifadhi fedha zetu ndani ya nyumba. Kuna watu hadi leo hii wanalala na fedha chini ya mito ya vitanda vyao wakiamini kuwa ziko salama, lakini si kweli. Mnachotakiwa kufanya ni kutumia huduma za kibenki kwani hata leo hii benki ikifilisika hela zenu mnazipata kwa mujibu wa sheria," alisema Samia.

Pia aliitaka benki ya Mkombozi na zingine kuhakikisha zinaangalia namna ya kuweka riba nafuu, ili kuwezesha vikundi na wafanyabiashara wadogo kukopa na kurejesha kwa urahisi.

"Suala la riba kwa wajasiriamali wadogo pamoja na wafanyabiashara wadogo bado ni changamoto sana. Benki nyingi bado zinariba za juu sana, hivyo basi niwaombe ninyi mwangalie namna ya kupunguza riba hiyo, lakini niwapongeze kwa kuwezesha vikundi kukopa kwa kujidhamini," alisema.

Makamu huyo wa Rais pia alizitaka benki na taasisi za kifedha nchini kubadili mfumo wa ujazaji fomu za kufungua akaunti kwa wateja ili kutumia lugha ya Kiswahili.

Alifafanua kuwa benki nyingi zimekuwa zikihamasisha wananchi kufungua akaunti kwa lugha ya Kiswahili na wakati mwingine hata kwa lugha mama ili kuwapata wateja, lakini jambo la kushangaza ni ujazaji wa fomu kutumia lugha ya Kiingereza.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mkombozi, Thomas Enock, alisema kuwa benki hiyo ilianzishwa miaka 10 iliyopota ikiwa na mtaji wa Sh. bilioni sita, lakini sasa umefikia Sh. bilioni 20.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera TFF kuendesha michuano ya yosso U-15

**WAKATI** zikiwa zimebakia siku sita ili kuanza kwa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019) huko Misri, tayari Tanzania imeanza maandalizi ya mashindano ya vijana ya umri chini ya miaka 17.

Timu ya Tanzania (Taifa Stars) ni moja kati ya mataifa 24 ambayo yatachuana katika fainali hizo zinazoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuwania kombe hilo linaloshikiliwa na Cameroon.

Taifa Stars inashiriki fainali hizo, baada ya kuzikosa kwa muda wa miaka 39, maana yake ilicheza mashindano hayo kwa mara ya mwisho mwaka 1980.

Lengo la Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kuandaa mashindano ya U-15 ni kutaka kuanza kusaka vipaji vipya ambavyo vitapeperusha bendera ya nchi katika michuano mbalimbali katika siku za hivi karibuni.

Uamuzi wa kuandaa au kuendesha mashindano hayo chini ya Rais wa shirikisho hilo, Wallace Karia, yametokana na kikosi chake cha Taifa cha umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys) kufanya vibaya kwenye Fainali za Afrika (Afcon U1-7), ambazo zilifanyika hapa nchini Aprili mwaka huu.

Serengeti Boys ambayo ilionekana kuwatoa kimasomaso Watanzania, ilishindwa kufurukuta mbele ya timu nyingine kutoka Afrika Magharibi na hata majirani zao, Uganda.

Matokeo hayo mabaya, yaliifanya TFF ikae chini na kutathimini, jambo jipya la kufanya ili kuandaa wachezaji ambao watalelewa kwa muda mrefu, ambao ndio wataibeba nchi katika mashindano ya kimataifa.

Gazeti hili linawapongeza TFF kwa kuandaa mashindano hayo, ambayo yanashirikisha timu kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani. Hii inaonyesha kuwa ahadi ya kuendeleza soka la vijana ambayo ilitolewa na Karia wakati ananadi sera zake kwa wajumbe wa mkutano mkuu wa shirikisho hilo, inatekelezwa kwa vitendo.

Ni wazi kuwa katika soka hakuna njia ya mkato, ili nchi au klabu yako iweze kufanya vema katika mashindano ya ndani au ya kimataifa ni lazima, viongozi wakubali kuwekeza.

Ili Stars iweze kuwa na makali ni lazima, TFF na klabu kukubali kuwekeza katika soka la vijana na ndani ya miaka michache ijayo, matunda yataanza kuonekana kwa kufanya vizuri kwenye mashindano mbalimbali ambayo Tanzania itashiriki.

Hakuna nchi ambayo imepata mafanikio katika soka au mchezo wowote bila ya kuwekeza katika ngazi ya vijana pamoja na makocha, kwa sababu hivi ni vitu viwili vinavyoendana ili kufikia maendeleo.


Nipashe inawapongeza TFF kwa kukubali kuanza kuwajenga wachezaji chipukizi ili ndoto za kubeba makombe mbalimbali ziweze kutimia, pia mikoa yote ambayo imeleta wachezaji ambao umri wao ni mdogo kama walivyoelekezwa.

Kuendesha mashindano ya vijana au ligi za wanawake ni gharama, kwa sababu hakuna kampuni ambazo zinajitokeza kudhamini michuano hiyo, lakini ni ukweli kuwa, mashindano ya vijana ndiyo yanayovumbua vipaji na yanayojenga wachezaji kwa kupitia mifumo sahihi.

Watanzania tunatakiwa tubadilike kwa kukubali kuwekeza katika michezo ya vijana, na hapo tutatarajia kuwa na wachezaji wenye viwango ambao watapeperusha vema bendera ya Tanzania kimataifa na jina la "Kichwa cha Mwenzawazimu" litabakia kuwa historia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Muhimu kwa wacheza kandanda

Na Barnabas Maro

**MPIRA** ni kitu cha mviringo kilichotengenezwa kwa mpira kwa ajili ya michezo; mchezo unaotumia kifaa kilichotengenezwa kwa mpira. Mpira wa miguu una majina mengi; kandanda, kabumbu, soka. Mingine ni mpira wa pete, mpira wa wavu na mpira wa magongo.

Zamani, kandanda ulikuwa mchezo wa kuwapa mazoezi wachezaji na wakati huo huo kuwaburudisha watazamaji. Wachezaji hawakulipwa hela kwani watazamaji waliingia viwanjani bure kufurahia mchezo huo.

Sasa mambo ni tofauti kwani mchezo wa kabumbu ni kazi kama zingine na wachezaji hulipwa mishahara, tena mikubwa kuliko hata wanaofanya kazi walizozisomea! Naam, "kila zama na kitabu chake."

Kuna methali isemayo "Kipendacho moyo ni dawa" kwamba kitu anachokipenda mtu au inachokipenda roho ya mtu huwa ni kama dawa yake. Methali hii hutumiwa kumpigia mfano mtu anayeelekea kukipenda kitu fulani sana ingawa wengine wanakiona kuwa cha kawaida au kibaya.

Hata kwenye kabumbu kuna baadhi ya wachezaji mahiri wanaovipenda mno vilabu vyao kiasi cha kutotaka kujitafutia hela zaidi kwenye vilabu vingine, ndani au nnje ya nchi. Labda baadhi yao huogopa kwenda nnje ya nchi kwa kutojua lugha ngeni. Hawapaswi kuogopa kwani tatizo hilo waachie miguu yao ndiyo itakayozungumza.

"Maendeleo" kwa muktadha ninaoujadili ni tendo la kutoka kwenye kiwango kidogo cha ufanisi na kufika kwenye kiwango kikubwa. Pia ni ongezeko la ubora katika huduma za kijamii kama vile elimu, uchumi, afya bora, mawasiliano n.k.

Hakuna asiyejua kuwa fedha, (pesa, hela au fulusi) ni sarafu inayotumika kulipia huduma mbalimbali zinazohusu maisha ya binadamu. Ndivyo wanavyotakiwa kujua baadhi ya wachezaji wetu wa kandanda wanaong'ang'ania kwenye vilabu vya nchini kwa kuvipenda mno badala ya kufikiria maisha ya kesho.

Mikataba ya wachezaji isiwe na upendeleo unaoegemea upande mmoja tu, yaani vilabu wanavyojiunga navyo au kuongeza mikataba baada ya awali kufikia ukomo. Wachezaji wanapaswa kuwa na wanasheria wa kutafsiri maana ya mikataba yao ili wasipunjwe masilahi yao au kubanwa na vilabu wanavyojiunga navyo.

Masilahi hayo ni mishahara itakayokubaliwa na pande zote mbili, kulipwa kwa wakati kwa kuwekewa kwenye akaunti zao za benki bila ubabaishaji kama ilivyo sasa. Ili kutimiza masharti hayo, wachezaji wawe na chama chao kitakachoendeshwa na wachezaji wastaafu kwani ndiwo wanaojua matatizo na stahiki za wachezaji. Kuwe na mwanasheria atakayesimamia mikataba ya wachezaji na vilabu.

Katika mikataba hiyo kuwe na kigezo (kielelezo, kipimo maalumu cha kufuatwa; sheria inayoongoza kutolewa uamuzi) kinachowapa wachezaji uhuru kujiunga na vilabu vingine vitakavyowapa masilahi mazuri zaidi. Mchezaji atakayeitumikia klabu yake kwa bidii, nidhamu na mafanikio apewe tuzo ya aina fulani na ikiwezekana aongezwe mshahara.

Aidha, vilabu viwekewe masharti ya matumizi ya fedha kwamba kila kinachonunuliwa kiwe na risiti inayothibitisha manunuzi. Kwa ufupi ni kwamba kila hela inayotoka klabuni iwe kwenye maandishi na ukaguzi ufanywe na wakaguzi wasiokuwa na tamaa ya hela ili wafanye kaguzi zao kwa haki bila ghiliba (udanganyifu wenye nia ya kujinufaisha).

Imebidi nitahadharishe mapema kwani baadhi ya viongozi hugombea nafasi hizo ili kujinufaisha kwa fedha za vilabu. Mfano mzuri ni kesi zilizo mahakamani inayowahusu waliokuwa viongozi wa chama kile kikuu kama ilivyo klabu fulani (nimesahau majina yao)!

Habari zisizo rasmi zaeleza kuwa kuna baadhi ya viongozi waliojenga nyumba kwa fedha za chama au vilabu vya mpira wanavyoviongoza. Ndio maana 'huwanunua' watu wa kuwafanyia kampeni kabla ya uchaguzi!

Hao wanaofanya hivyo, watafakari kwa kusoma methali hii: "Penye urembo ndipo penye ulimbo." Mahali penye urembo huwa pana mtego unaoweza kukunasa. Methali hii hutumiwa kumnasihi mtu asikiendee kitu fulani kwa pupa kwa kuwa kinamvutia kwa sababu huenda kikawa na madhara fulani baadaye. Hutukumbusha umuhimu wa kuvichunguza vitu kwanza.

Vilevile vilabu vyapaswa kuwakumbuka wachezaji wao waliostaafu wanapopata maradhi hata kutoweza kujitibu. Kuna wachezaji wengi wa vilabu vikubwa nchini, hasa vya Simba na Yanga walioviletea vilabu hivyo sifa kubwa ndani na nje ya nchi, lakini sasa hawathaminiwi wala kukumbukwa! Au ndio yale yasemwayo "yaliyopita yamepita?"

"Asante tupu haijazi chungu." Shukrani au asante isiyo na kitu haijazi chungu. Tuwafariji waliofikwa na maafa fulani kwa vitendo wala sio maneno matupu tu.

## HABARI KITAIFA

# Biteko kufungua soko la kimataifa la madini

**Novatus Makunga,** ARUSHA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, leo anatarajia kufungua soko la kimataifa la madini katika jijini Arusha, likiwa ni la pili baada ya la mpakani mwa Tanzania na Kenya katika eneo la Namanga.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, aliiambia Nipashe mjini hapa kwamba soko hilo litakuwa katika jengo ambalo hapo awali lilikuwa likitumiwa na shule ya Braeburn katika barabara ya Old Moshi.

"Hatua ya kufungua soko hilo imezingatia mahitaji ya wadau wa madini kwa maana wachimbaji wa madini, wanunuzi wakubwa na wafanyabiashara wa kimataifa kutoka nchi mbalimbali ambako shughuli kufanyikia hapo ni rahisi kwao, usalama wa uhakika na miundombinu muhimu yote ipo," alisema.

Gambo alisema kuwa soko hilo litakuwa umbali mfupi kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), eneo lenye huduma zote za kibenki na hoteli ya ngazi mbalimbali.

Kaimu Ofisa wa Madini Mkazi wa Arusha, Robert Erick, alisema uamuzi wa kufungua soko la kimataifa la madini jijini Arusha unatokana na mji huo kuwa kitovu cha madini ya aina mbalimbali ya vito.

Erick alisema soko hilo ni la pili kuanzishwa mkoani Arusha baada ya mwezi Aprili, mwaka huu, kufunguliwa soko lingine katika eneo la Namanga ambako ni mpakani mwa Tanzania na Kenya.

Alisema soko hilo la Namanga limekuwa likifanya kazi katika siku zote za kazi kuanzia Jumatatu mpaka Ijumaa na imewalazimu wadau wa madini kusafiri kutoka mjini kwenda umbali wa zaidi ya kilometa 100.

Akifafanua faida ya kuwapo kwa masoko hayo, Erick alieleza kuwa kwa kiasi kikubwa imepunguza utoroshaji wa madini kupitia njia za panya pamoja na urasimu kwa wauzaji na wanunuzi wa madini.

Aidha, Erick alisema kuwa utaratibu huo umerahisisha upatikanaji wa kodi za serikali pamoja na ukusanyaji wa takwimu za madini.

"Ni mfumo ambao unawasaidia hata wanunuzi na wauzaji kutapeliwa kama ilivyo kuwa siku za nyuma, lakini pia kuwaondolewa usumbufu wa kuzunguka kutoka ofisi moja hadi nyingine na pia kutusaidia kukusanya maduhuli ya serikali," aliongeza.

Baadhi ya madini ya vito yanayopatikana mkoani Arusha ni pamoja na Tanzanite, Sapphire, Emarald, Tourmaline, Aguamarine, Zircon, Garnet, Arnethyst, Rhodolite na Alexandrite.

Ufunguzi wa masoko ya madini katika maeneo mbalimbali unatokana na agizo la Rais John Magufuli, alilolitoa Aprili 27, mwaka huu alipokuwa wilayani Chunya.

Akiwa wilayani humo, Rais Magufuli alitoa siku saba kwa wakuu wa mikoa yote yenye shughuli za uchimbaji wa madini kuhakikisha wanafungua masoko hayo.

# Mbaroni tuhuma mauaji kada wa Chadema

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za mauaji ya mkulima na Katibu Mwenezi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), wilaya ya Malinyi, Lucas Luhambalimo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa awali, Luhambalimo (42) alikuwa na ugomvi na mkazi mmoja wa eneo hilo, Francis Kologaki, maarufu kama Mwanampalu wa kijiji cha Munga wilayani Malinyi, ambaye ni miongoni mwa watuhumiwa waliokamatwa kuhusika na mauaji hayo.

Mbali na Kologaki, watuhumiwa wengine ni Robson Mgeni na Memory Mbegalo, wote wakazi wa Mtimbira na kwamba uchunguzi wa awali umebaini chanzo cha mauaji hayo kulipiza kisasi kutokana na mgogoro wa mashamba.

Alisema uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa kulikuwa na ugomvi baina ya watu hao na Septemba 3, mwaka jana, Luhambalimo alimshtaki Kogolaki kwa madai ya shambulio katika Mahakama ya Mwanzo Mtimbira. Katika kesi hiyo, Kagolaki alihukumiwa kwenda jela miezi mitatu au kulipa faini ya Sh. 50,000 na alilipa fedha hizo.

Baadaye Desemba 3, mwaka jana, Kogolaki na wenzake wawili walifunguliwa kesi ya madai katika Baraza la Ardhi la Kata, wakati huo Luhambalimo akiwa shahidi wa shauri hilo na ilitakiwa Juni 13, mwaka huu, afike barazani hapo kwa ajili ya kutoa ushahidi.

Hata hivyo, alisema siku ya tukio majira ya usiku wa manane, katika kijiji cha Munga, Luhambalimo ambaye alikuwa na wake wawili, Anastazia Sandi (42) na Zaituni Matandiko (42), alikuwa amelala kwa mke (Zaituni). Ghafla alisikia vishindo vya watu wakitembea nje ya nyumba yao na alimwamsha mkewe na kumjulisha juu ya hali hiyo.

Kamanda Mutafungwa alisema Luhambalimo aliamua kuchungulia nje kupitia uwazi wa ukuta na kwa msaada wa mbalamwezi, aliwaona watu watatu na kumtambua Francis Kogolaki akiwa ni miongoni mwa watu hao.

Kutokana na hali hiyo, alimjulisha mkewe juu ya watu hao, ambao walizunguka upande mwingine wa nyumba na mwanamume huyo akawafuata upande huo tena kuchungulia, lakini ukasikika mlipuko mithili ya bunduki.

"Mwanaume yule (marehemu) akarudi kwa mkewe akiwa anavuja damu kichwani na akamweleza alipigwa na watu wale na mke alipochungulia tena nje kwenye uwazi, aliwaona watu wale watatu akiwamo mmoja aliyemtambua kuwa ni Francis wakiondoka eneo la nyumbani kwao," alisema Kamanda Mutafungwa.

Alisema baada ya tukio hilo, mwanamke huyo alipiga kelele za kuomba msaada na majirani walijitokeza na walipopewa taarifa kuhusu watu wale watatu walioonekana, walijaribu kuwafuatilia na kuwatafuta bila mafanikio, hivyo kumchukua Luhambalimo na kumpeleka katika Kituo cha Afya cha Mtinmbira kwa ajili ya matibabu.

Hata hivyo, alipoteza maisha akiwa njiani na wananchi wakafikisha taarifa katika kituo cha polisi. Kamanda alisema kutokana na tukio hilo, polisi waliendesha msako mkali kwa kushirikiana na wananchi na hatimaye kuwakamata watuhumiwa. Watuhumiwa hao, alisema wote watafikishwa mahakamani kujibu mashtaka yanayowakabili.



Mkuu wa Kitengo cha Uchunguzi wa Silaha na Milipuko cha Jeshi la Polisi nchini, Mrakibu Msaidizi wa Polisi John Mayunga, akitoa elimu kuhusu silaha na milipuko kwa sehemu ya askari 300 wa Chuo cha Kijeshi Pangawe Morogoro, walipofanya ziara ya mafunzo katika Kamisheni ya Uchunguzi wa Kisayansi, iliyopo Makao Makuu ya Jeshi hilo, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Polisi wamwita aliyewatuhumu

**INATOKA UK. 3**

Katika barua yake, Moshi alidai kuwa Mei 14, mwaka huu, akiwa mkoani humo alikwenda kwenye duka la fedha akiwa na Sh. 1,630,000 kwa ajili ya kuwekewa fedha hizo kwenye simu lakini mhudumu alimwambia kuwa ana Sh. 600,000 kwenye simu yake.

"Nilimkabidhi mhudumu wa M-Pesa Sh. 600,000 akadai bado Sh. 5,000, nilipompa kabla hajaniwekea fedha kwenye simu yangu alitoka nje ya duka na aliporudi alikuwa ameambatana na mlinzi wa benki ambaye ni JKT Suma, yule mhudumu akasema mimi ni mwizi nataka kumwibia nimempa fedha pungufu," ameandika Moshi.

Katika barua hiyo, Moshi amedai kuwa simu ilipigwa polisi na walifika askari na kumchukua kuelekea kituoni.

"Pale pale askari waliniuliza nina shilingi ngapi, nikawajibu jumla ni Sh. 1,630,000 na nikitoa nilizomkabidhi mhudumu wa M-Pesa, nilizo nazo mfukoni ni Sh. milioni 1,030,000," aliandika.

Moshi aliendelea kudai kuwa waliondoka na askari hao ambao walijitambulisha kwa majina bandia, Lyimo wakati ni Novatus, Dula wakati ni Abdalah na watatu ambaye hakujitambulisha.

"Askari hawa hawakunipeleka mapokezi ya kituo cha polisi waliniingiza kwenye vyumba ambako ni karibu na kituo cha polisi vimepakana na ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Mkoa (RCO), walinipekuwa hawakuandika PPR ili isijulikane kiasi nilichokuwa nacho.

"Walichukua maelezo na baadaye wakaniambia Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD) anazitaka fedha. Wakanirudishia Sh. 442,000. Hawakunifungulia kesi yoyote wakaniambia nijidhamini kwa Sh. 500,000 ya maneno, wakaniruhusu nikaondoka."

Moshi alidai kuwa Mei 15, aliamua kuwasiliana na Kamanda wa Polisi wa mkoa huo pamoja na RCO ili wamsaidie ndipo walipomwambia aende kwa OCD.

"Nilikwenda kwa OCD na askari wale walipatikana na RCO akasema ufanyike uchunguzi na kazi hiyo alipewa askari Sajenti Christopher (ametaja namba yake ya simu), baada ya uchunguzi RCO akaamua kuwa askari hao wasirudishe fedha na akachukua simu yangu kuwa wanaifanyia uchunguzi, nilisubiri majibu kila nikipiga simu kwa Christopher akawa hapokei," ameandika.

Moshi ameandika kwenye barua hiyo kuwa kutokana na hali hiyo aliamua kurudi Dar es Salaam na ameomba vyombo husika kufuatilia ili arudishiwe fedha zake Sh. milioni 1,188,000 pamoja na alizotumia kusubiri wakati wote kiasi cha Sh. 990,000.

Nipashe ilipomtafuta Sajenti Christopher ili kujua kama anafahamu suala hilo alisema hafahamu tukio hilo wala mtu huyo na kumuomba ni vyema aende Mwanza, ili wakutane amuone.

"Yeye anasema alikuwa Mwanza akaondoka, aje Mwanza sizijui habari hizi unazoniambia kama kulikuwa na mkwamo kwa nini asirudi kwa RPC, simfahamu wala kesi siifahamu," alisema.

# Anusurika kifo kwenye uzazi

INATOKA UK. 2

kuwa gari halina mafuta," alisema Nangi.

Alisema akiwa amevaa gloves aliendelea kumwambia ndugu wa Belinda kutafuta jina la mratibu wa afya ya uzazi na mtoto wa wilaya hiyo, ambaye alifanya jitihada za kutafuta mafuta na kwenda haraka zahanati hapo na kumchukua mzazi huyo aliyekuwa ameshapoteza fahamu na kumfikisha kwenye hospitali kubwa ya misheni ili kuokoa maisha ya Belinda.

Kwa upande wake Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto wilayani hapa, Neema Mwijarubi, alisema siku hiyo kulikuwa na sherehe ya wauguzi Musoma mjini, lakini yeye hakujisikia kwenda alikuwa amelala nyumbani kwake na kushtushwa na simu muda wa saa tano usiku kuwa kuna mzazi amezidiwa na gari la wagonjwa halina mafuta.

"Kweli gari lilikuwa halina mafuta ila tulijitahidi tukaweka, lengo tuweze kuokoa maisha ya huyu mama, maana baada ya kufika pale niliona damu imejaa ndoo nikamuuliza yule muuguzi kama aliongeza maji akasema hapana zilikuwa damu na niligundua alikuwa amechanika, pia damu ilikua ni Hb 3 ambayo ni kiwango kidogo sana," alisema Mwijarubi.

Alisema wakiwa njiani kumkimbiza huyo mzazi hospitali kubwa ya misheni Kowaki, Belinda alikuwa amepoteza fahamu, huku upumuaji ukiwa chini hali iliyomfanya aagize waandae mashine ya oxygen na walipomfikisha akiwa na dripu mbili za maji baadaye walimuongeza damu dripu tatu na saa tisa usiku Belinda alirejewa na fahamu zake kama kawaida na siku iliyofuata aliruhusiwa kurudi nyumbani.

Mganga Mfawidhi wa zahanati hiyo, Blacius Mganyizi, alisema zahanati hiyo inakabiliwa na upungufu wa watumishi ikiwa na wafanyakazi sita pekee.

Aliiomba serikali kuongeza majengo kwa kuwa kwa sasa kuna chumba kimoja cha wajawazito kujifungulia.

Kufuatia tukio hilo Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adamu Malima, alitoa zawadi ya Sh. milioni moja kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya afya kuitoa kwa wauguzi wote waliopambana kuokoa uhai wa Belinda na mtoto wake.

"Kwa mujibu wa takwimu za Tanzania Demographic Health Survey (TDHS) ya mwaka 2015/16 katika mkoa wa Mara, wajawazito waliojifungulia kituoni ilikuwa ni asilimia 50 chini ya kiwango cha taifa ambacho ni asilimia 63, wazazi waliosaidiwa na watoa huduma wenye ujuzi walikuwa ni asilimia 51 chini ya kiwango cha taifa ambacho ni asilimia 64," alisema.

# Muhimbili yaanza kuondoa uvimbe bila upasuaji

INATOKA UK. 2

wa sampuli kutoka kwenye uvimbe sehemu mbalimbali za mwili ambazo si rahisi kufikiwa bila upasuaji mkubwa.

Dk. Lwakatare alisema walizibua mirija ya nyonga, kuweka mirija kwenye figo, mirija ya mkojo iliyoziba na unyonyaji wa uvimbe wenye maji na usaha ikiwa ni mwendelezo wa huduma hiyo.

Alisema tiba hiyo inafaida inawezesha kuepuka upasuaji mkubwa ambao una vihatarishi, kuepuka kukaa hospitali kwa muda mrefu kwa kuwa wanaofanyiwa tiba hiyo ya radiolojia mara nyingi hurudi nyumbani siku hiyo hiyo.

"Hii tiba inapunguza gharama kwa mgonjwa maana ukishapatiwa matibabu unaondoka siku hiyo hiyo sio kwamba utalazwa," alisema.

Alisema kipindi cha nyuma tiba hizo huwa zinahitaji upasuaji mkubwa na kulazwa hospitalini kwa muda mrefu.

Aidha, alisema tangu waanzishe huduma hiyo wagonjwa 339 wamepatiwa huduma ya kibingwa ya tiba radiolojia wengi wakiwa wagonjwa wenye uvimbe kinywani. Alisema wagonjwa wenye uvimbe wa kinywa walikuwa wakipelekwa nchini India kutibiwa kwa gharama ya Sh. milioni 99, kwa sasa Hospitali ya Muhimbili wanaitoa kwa Sh. milioni mbili.

Aidha, alisema wamepatiwa ujuzi mpya wa kuweka mipira maalum kwenye mishipa mikubwa ya damu ambayo itawanufaisha wagonjwa wa figo walio kwenye mfumo wa kusafisha damu au wanaopatiwa tiba ya saratani.

Dk. Newsome alisema wamekuja kubadilishana uzoefu na madaktari wa Tanzania na suala la muhimu ni kushirikiana ili kutekeleza majukumu yao.

**Baadhi ya dalili za uvimbe (Fibroids)**

- Kutokwa damu kwa wingi wakati wa siku za hedhi au kwa muda mrefu.
- Kutokwa damu kusiko kwa kawaida katikati ya siku za mwezi au maumivu ya nyonga (uvimbe kugandamiza kwenye viungo vya nyonga)
- Kupata haja ndogo mara kwa mara, maumivu ya mgongo, maumivu wakati wa tendo la ndoa, upungufu wa damu.
- Maumivu ya kichwa, maumivu kwenye miguu, kuvimba sehemu ya chini ya tumbo (Fibroids kubwa), uzazi wa shida, mimba za shida, kutopata mimba na kutoka kwa mimba mara kwa mara.

Wanawake wengine wenye uvimbe wa fibroids huwa hawaoni dalili zozote (wengi hawajui kama wana fibroids) au kuona dalili kidogo na kwa wengine dalili hizi hujitokeza sana na kuwasumbua hadi kufikia kutafuta tiba. Fibroids ni nini

Kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali, Fibroids ni uvimbe wa misuli laini wenye mizizi ya kuiunganisha unaoota na kukua kwenye uterus.

Fibroids ni aina ya uvimbe unaoonekana kwa wingi zaidi katika mfumo wa uzazi wa mwanamke na mara nyingi asilimia 99 hauna madhara kiafya na wala kuhusiana na ugonjwa wa kansa.

Inakadiriwa kuwa kati ya asilimia 20 hadi 50 ya wanawake walio katika umri wa kuzaa, miaka 30 hadi 50, wana fibroids ingawa wengi wao hawahangaiki kuchukua vipimo vya fibroids.

Uvimbe wa fibroids unakuwa na ukubwa tofauti tofauti, unaweza kuwa mdogo kama harage au kufikia ukubwa wa tikiti maji.

# Mishahara, madeni yalamba tril. 12/- ndani ya miezi 10

INATOKA UK. 2

mikopo hiyo kwa gharama zinazohimilika," alisema. "Mwenendo wa upokeaji wa upatikanaji wa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo ulikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo baadhi ya washirika wa maendeleo kutotimiza ahadi zao kama walivyoahidi kwenye bajeti, kinyume cha misingi ya makubaliano yaliyoainishwa kwenye Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo Tanzania (DCF), " alisema.

**TRIL. 12/- MISHAHARA, MADENI**

Dk. Mpango alibainisha kuwa kati ya Sh. trilioni 22.19 zilizotolewa na serikali hadi kufikia Aprili mwaka huu, Sh. trilioni 6.3 zimetumika kulipa mishahara ya watumishi, ikiwa ni wastani wa Sh. bilioni 630 kwa mwezi.

Waziri huyo pia alisema serikali iliendelea kulipa madeni yake kwa mujibu wa mikataba, akibainisha katika kipindi hicho cha miezi 10, Sh. trilioni 5.7 zilitumika, ikiwa ni wastani wa Sh. bilioni 570 kwa mwezi.

Kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Dk. Mpango alisema jumla ya Sh. trilioni 5.44 zilikuwa zimetolewa.

Aprili mwaka jana, waziri huyo aliwaambia waandishi wa habari bungeni jijini Dodoma kuwa serikali imekuwa ikishindwa kupeleka fedha nyingi kwenye miradi ya maendeleo inayoidhinishwa na Bunge kutokana na kiwango kikubwa cha makusanyo yake kutumika kulipa mishahara ya watumishi wa Umma na Deni la Taifa.

# Bajeti yapongezwa kila kona

INATOKA UK. 3

bajeti ya mwaka 2019/20 ni tofauti na bejeti zilizopita kwa kuwa imeeleza inakwenda kutekeleza masuala ambayo yanawagusa kundi kubwa la Watanzania.

"Kupunguzwa kwa kodi nyingi kwa wafanyabiashara imedhihirisha kuwa serikali imekuwa ikisikiliza maoni ya sekta binafsi, imefuta na kurekebisha mifumo ya kodi ambayo ilikuwa ni kandamizi," alisema Prof. Semboja.

Hata hivyo, Prof. Semboja alitoa angalizo kwa serikali akiitaka kutotegemea vyanzo vya kodi peke yake katika kuendesha mambo yake, bali iangalie vyanzo vingine.

Rais wa Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (Tucta), Tumaini Nyamuhokya, alisema licha ya kuwa ni bajeti ambayo imegusa kundi kubwa la wafanyabiashara, imemsahau mfanyakazi.

"Sisi kwetu bado ni pigo. Tunawaomba wabunge watusaidie, kama wameona kuwakumbuka wafanyabiashara walipaswa kuwakumbuka na wafanyakazi ambao ndio wengi," alisema Nyamhokya.

Alisema licha ya kodi nyingi kupunguzwa, bajeti hiyo imesahau kupunguza PAYE ambayo imekuwa ikipigiwa kelele miaka mingi.

Katibu Mkuu wa Chama cha Mawakala wa Forodha Tanzania (Taffa), Tony Swai, alisema bajeti imegusa maeneo mengi mazuri, lakini utaratibu wa kuondoa mawakala wa forodha hautakuwa jambo jema.

Alisema mawakala wa forodha wanatambulika na Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ya Afrika Mashariki ya mwaka 2009 kifungu cha 145 (1) (2) pamoja na kifungu cha 146.

Swai alisema kuondolewa kwa mawakala hao kunaweza kusababisha zaidi ya watu 10,000 kupoteza ajira.

# Aliyehukumiwa kunyongwa

INATOKA UK. 4

hakusikilizwa na wala utetezi wake haukuzingatiwa katika rufani hiyo.

Akifafanua zaidi alidai kuwa Mahakama ilisikiliza ushahidi wa DPP ikaacha utetezi wa Bageni na kwamba ametiwa hatiani na kuhukumiwa adhabu hiyo kwa ushahidi ambao haupo.

"Ukiangalia rufani ya DPP katika ushahidi wa mashahidi 37 wa Jamhuri na 13, wa utetezi hakuna ushahidi uliomgusa Bageni, mahakama hii ilipomtia hatiani imepoteza haki yake naiomba mahakama isiruhusu tena ukiukwaji huu wa haki," alidai Ishengoma wakati akihitimisha hoja za maombi ya mlalamikaji.

Upande wa mlalamikiwa DPP ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladislaus Komanya, ulidai kuwa mlalamikaji hana sababu za msingi za kutengua uamuzi uliomtia hatiani.

Komanya alidai kuwa rufani ya kesi hiyo ilishasikilizwa kwamba sasa si wakati wake kusikilizwa kwa mgongo wa mapitio. Alidai kuwa Bageni alipata nafasi ya kusikilizwa na kwamba mahakama itupilie mbali mapitio hayo.

"Mahakama hii ina uwezo wa kusikiliza jambo na kulifanyia uamuzi kwa hiyo mambo yatakayoletwa yazingatie kifungu cha 66 kidogo cha (1) (b) cha kanuni ya adhabu, maombi ya mlalamikaji tunaona hayajakidhi vigezo vinavyotakiwa, kwa kuruhusu maombi kama haya ambayo hayafiki mwisho tunafungua mwanya kwa wengine yatupiliwe mbali," alidai Komanya.

Ishengoma alikijibu hoja za mlalamikiwa alidai kuwa si sahihi na kwamba kifungu cha 66 (1) (b) hakijakidhi vigezo vya kupiga mapitio hayo na kwamba mtuhumiwa kama Bageni ambaye alitiwa hatiani na Mahakama ya Rufani na hana kwingine kwa kukimbilia kudai haki yake.

Alidai kuwa mapitio haya ni tofauti na mengine ambayo mtuhumiwa ametiwa hatiani na Mahakama ya chini.

Aidha, jopo hilo lilisema baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili mahakama inakwenda kuzifanyia kazi na pande hizo zitajulishwa tarehe ya uamuzi.

Katika maombi yake SP Bageni anapinga hukumu iliyotolewa katika mahakama hiyo chini ya jopo la majaji watatu likiongozwa na Jaji Bernard Luanda, Sauda Mjasiri na Senistocles Kaijage kwamba lilifanya makosa ya dhahiri.

Pia, anadai kuwa jopo hilo lilifanya makosa katika mwonekano na kusababisha haki kutokuzingatiwa mahakama hiyo itenguwe hukumu hiyo.

# Viongozi wa dini wakumbushwa haki na amani

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

VIONGOZI wa dini nchini wamekumbushwa umuhimu wa kuhubiri amani na haki katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani ili vifanyike kwa amani.

Meneja Miradi wa Shirika lisilo la kiserikali la Maendeleo ya Watu wa Marekani (IRI), Elly Ahimidiwe, alisema hayo jana katika semina ya viongozi wa madhehebu ya dini lililofanyika hoteli ya Naura Spring.

Alisema shirika hilo limekuwa likihusika na miradi mbalimbali katika jamii ikiwamo kutoa mafunzo kwa viongozi wa dini na kuwajengea uwezo viongozi wa vyama vya siasa, lengo likiwa kukuza demokrasia katika dhana ya utawala bora na hadi sasa limezifikia nchi 35.

Ahimidiwe alisema kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Septemba, mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani, viongozi wa dini wana nafasi kubwa kwa waumini wao katika kuihubiri amani na kuishauri kamati ya ulinzi na usalama ili kudumisha amani pande zote.

Pia aliwataka viongozi wa dini kuheshimu sheria za nchi na kufanya kazi zao pasipo uvunjifu wa amani.

"Amani ni muhimu hasa katika kipindi tunachokiendea cha uchaguzi. Nyie mna nafasi kubwa ya kuhubiri amani na haki ila zingatieni sheria za nchi katika utendaji wenu wa kazi," alisema.

Mkurugenzi wa Baraza la Amani Tanzania Askofu Mkuu wa Kanisa la Rehoboth Victory, Nasson Ngoingoi, alisema ni wakati sasa wa kushirikiana na kuzitatua tofauti zilizopo ili kujenga umoja wa kitaifa.

Naye Katibu wa Kamati ya Amani Mkoa wa Arusha, Abdallah Masoud, alisema viongozi wa dini wamekuwa watu wa karibu ndani ya jamii licha ya kukutana na changamoto nyingi katika madhehebu yao.

"Mnapaswa kuwa na upeo mkubwa na jukumu la kuhudumia waumini wenu bila ubaguzi ili kuitunza amani ambayo ndiyo tunu iliyoachwa na viongozi waliotangulia," alisema.

Hata hivyo, Sheikh wa Mkoa wa Arusha, Shabani Juma, alisema viongozi wa dini wanapaswa kuendeleza kamati hizo na kuzishauri pale mambo yanapoonekana kuyumba ili kuleta umoja wenye tija.

Mkurugenzi wa Baraza la Amani Tanzania, Askofu Thomas Godda, alisema kuwapo kwa chombo hicho kumetoa fursa ya kurekebishwa kwa kasoro zilizokuwa zikijitokeza katika miaka iliopita kwa kuwa walikosa



Mbunge wa Jimbo la Simanjiro mkoani Manyara, James Ole Millya (wapili kushoto), akikagua mradi wa maji kwenye Kijiji cha Terrat, wilaya hiyo imechimba visima 20 katika vijiji mbalimbali, kulia ni Diwani wa Terrat, Jackson Ole Mater. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wajawazito wahofia ufa jengo la uzazi

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

WANAWAKE wanaokwenda kujifungua katika zahanati ya Nadonjukin iliyoko katika Kata ya Komolo wilayani Simanjiro mkoani hapa, wamekumbwa na hofu juu ya usalama wao kutokana na chumba cha kujifungulia kuwa na ufa mkubwa.

Zahanati hiyo ambayo inahudumia zaidi ya wakazi 3,000 wa kata hiyo, pia inakabiliwa na uhaba mkubwa wa dawa kutokana na kutosajiliwa kwenye mfumo rasmi wa namna ya kudhibiti dawa zinazoingia na kutoka. Akizungumza juzi mbele ya Mbunge wa Simanjiro, James ole Millya, wakati wa siku ya pili ya ziara yake jimboni humo akiwa ameongozana na wakuu wa idara wa halmashauri ya wilaya hiyo, Mganga Mkuu wa Zahanati hiyo, Joseph Mungaya, alisema jengo hilo liko hatarini kubomoka kutokana na nyufa nyingi na kubwa ambazo zinaweza kuhatarisha maisha ya wagonjwa. "Ninapokuwa chumba cha kuzalishia wanawake huwa napata wakati mgumu, huku nikimuomba Mungu tutoke salama kutokana na ufa mkubwa ambao unasababisha hata mjamzito kuwa na hofu kubwa wakati wa kujifungua," alisema.

Licha ya changamoto hiyo, Mungaya pia alisema yeye na familia yake wanaishi kwenye chumba kimoja ndani ya zahanati hiyo kwa zaidi ya mwaka sasa kutokana na kutokuwapo kwa nyumba ya daktari na kwamba katika Kijiji hicho hakuna nyumba yoyote ya kupangisha.

"Familia yangu iko hatarini kupatwa na mgonjwa ya mlipuko kwa kuwa tunaishi hapa ndani ya zahanati, lakini pia tunakabiliwa na upungufu wa wauguzi watano," alisema.

Naye mmoja wa wanawake waliokuwa katika zahanati hiyo kwa ajili ya kujifungua, Einot Laizer, alisema anamwomba Mungu atoke salama katika chumba hicho kwa kuwa anapatwa na hofu kila akilala na kuangalia ufa huo mkubwa ambao umeacha nafasi kubwa kiasi cha kuona upande wa pili.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Isaya Saikoon, alisema ujenzi wa nyumba ya muuguzi imeghubikwa na ufisadi mkubwa kwa sababu imeshatumia Sh. milioni 4.6 kwa ujenzi wa msingi pekee licha ya wananchi kujitolea michanga, moramu, mawe na Sh. milioni 1.6.

Alisema licha ya fedha hizo, pia Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Charles Chaula, alitoa mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya ujenzi huo pamoja na Ofisi ya Mbunge ambayo ilitoa Sh. milioni tatu, lakini fedha zote hizo zimeishia kwenye ngazi ya msingi pekee.

Akijibu changamoto hizo Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Celestine Silayo, alikiri zanahati hiyo kutokuwa kwenye mfumo wa serikali kwa ajili ya kupatiwa dawa na kwamba na mganga mkuu wa wilaya ameshapeleka maombi Wizara ya Afya ili zahanati hiyo iingizwe kwenye mfumo.

# Longido wamwaga pongezi kwa Rais

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANANCHI wa Wilaya ya Longido wamemshukuru Rais John Magufuli kwa kutoa Sh. bilioni 1 .5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya.

Hospitali hiyo ambayo inatarajia kuwekwa mabati, milango na madirisha Juni 30, mwaka huu, itawaondolea adha wananchi ya kutembea zaidi ya kilomita 75 kufuta huduma za afya hasa wale wa kutoka vijijini.

Wakitoa shukrani zao jana mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, ambaye alifika eneo hilo juzi akiongozana na kamati ya ulinzi na usalama, baadhi ya wananchi hao wakiwamo Jumanne John na Isaya Mollel, walisema uwapo wa hospitali hiyo utawasaidia kutatua changamoto za afya ikiwamo kupunguza gharama za kufuata matibabu mkoani Arusha.

"Tunamshukuru Rais Magufuli kwa kutujengea kituo hiki kwani hatukuwa na hospitali ya wilaya tulikuwa tunateseka. Awali tulifuata huduma hii katika Hospitali ya (Rufani ya) Mkoa ya Mount Meru, lakini sasa tutapata huduma hapa hapa," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Jumaa Mhina, walisema hospitali hiyo ina majengo saba likiwamo la wagonjwa wa nje.

Walisema hospitali hiyo itawezesha wananchi kuondokana na adha ya kusafiri umbali mrefu kwenda kufuata huduma za afya mkoani Arusha.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya hiyo, Franck Mwaisumbe, alisema awali walikumbana na changamoto ya uhaba wa mbao, milango ambayo ni lazima waagize kutoka mkoani Iringa, lakini licha ya changamoto hiyo Mkurugenzi Mhina pamoja na watendaji wa halmashauri wamehakikisha kituo hicho kinaisha ili kianze kutoa huduma kwa wananchi.

Mhina alisisitiza kuwa saruji wanayoitumia katika ujenzi huo ni ile inayodumu kwa muda mrefu.

Pia alisema hospitali hiyo itawasaidia kinamama na watoto wanaoteseka kupata huduma za afya katika wilaya hiyo, huku wengine wakijifungulia nyumbani kutokana na kutembea umbali mrefu.

"Lakini hivi sasa ujenzi wa hospitali hiyo utakapokamilika utawasaidia kupata huduma bora za afya na kupunguza umbali mrefu wa kwenda Hospitali ya Mount Meru iliyoko jijini Arusha," alisema.

# Ataka vijana wapewe ajira kupitia taka

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI mkoani Kilimanjaro imeitaka Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kuibua ajira mpya kwa vijana kwa kuwapa fursa ya kukusanya taka kwenye makazi ya watu kibiashara na kupeleka katika eneo maalumu litakalotengwa badala ya mfumo unaotumika sasa.

Kwa sasa manispaa inapitisha gari mitaani kubeba taka, jambo linaloweza kufanywa na vijana hao na kupeleka katika kituo maalumu ambacho kitatumiwa kubeba kwa pamoja na kupeleka dampo kuu.

Katibu Tawala Msaidizi (AAS), Utawala na Rasilimali Watu wa mkoa, Bwai Biseko, alisema hayo jana alipokuwa akifungua kikao cha mazingira kilichojumuisha viongozi wa mitaa na kata zinazozunguka msitu wa Rau ili kuondoa tatizo la utupaji taka katika msitu huo.

"Vijana wanaweza kutumika baada ya jamii kuchangia kiasi fulani cha fedha ili taka zirundikwe eneo moja, huku magari ya manispaa yakipita kukusanya katika vituo vikuu. Hili linawezekana kama jamii itakuwa na dhamira ya dhati kubadilika katika usafi wa mazingira," alisema.

Biseko alisema lengo la mipango hiyo ni kuhakikisha msitu wa Rau unatumika kama sehemu ya utalii, lakini pia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi yanayosababisha athari za uharibifu wa mazingira.

Naibu Meya wa Manispaa hiyo, Jomba Koyi, alisema manispaa ina mipango ya kugeuza taka kuwa rasilimali kwa ajili ya uzalishaji wa gesi.

"Tayari tumetangaza zabuni ya ujenzi wa dampo jipya eneo la Mtakuja nje ya Manispaa na hadi Desemba, mwaka huu, taka zitakuwa mali na wananchi watauza taka zao badala ya kuzitupa.

Hii itabadili mtazamo na itatunza mazingira," alisema.

Naye Ofisa Maliasili wa Mkoa, Emanuel Kiengi, alisema kikao hicho kilichoendeshwa kwa ufadhili wa Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), kimelenga kuhakikisha sheria, taratibu na mamlaka zinazosimamia misitu vinaheshimika.

Alitaka viongozi hao kubeba dhamana ya kulinda rasilimali za msitu huo kwa kutoa elimu kwa jamii inayouzunguka ili kuuhifadhi.

Awali, Ofisa Misitu wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Joshua Mungure, alikiri kuwapo kwa uchafu wa taka ngumu na nyinginezo katika msitu wa Rau, jambo ambalo halikubaliki na kutaka jamii kubadili tabia.



Diwani wa Kata ya Bomambuzi, Manispaa ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro, Juma Raibu, akishiriki kazi za kijamii kwa kuzibua mitaro ya majitaka katika kata yake juzi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Waonywa kuhusu hatari ya umeme

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANANCHI wametahadharishwa kujiepusha kufanya biashara chini ya miundombinu ya umeme hasa katika kipindi cha mvua ili kuepuka madhara mbalimbali yanayoweza kuwapata.

Rai hiyo ilitolewa jana na Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) Mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi Mahawa Mkaka, alipozungumza na gazeti hili ofisini kwake.

Alisema vitendo vya ufanyaji wa biashara chini ya miundombinu ya umeme vinaweza kuhatarisha maisha kwa watu wanaofanya shughuli katika maeneo yenye miundombinu ya umeme.

Mhandisi Mkaka alisema kipindi hiki cha mvua miundombinu imekuwa ikiharibika kutokana na upepo mkali huku pia mvua hizo zimekuwa zikiendana na radi, jambo ambalo ni hatari pindi wananchi wakiendelea kufanya biashara chini ya miundombinu hasa transifoma.

Meneja huyo alisema kutokana na madhara hayo, ni vyema wananchi wakajijengea tabia ya kuvaa viatu na kuepuka kukanyaga maji ovyo kwa kuwa umeme unasafiri kwa kasi ndani ya maji.

"Nawasihi sana wananchi ili kuepukana na kupigwa na shoti ni vyema basi wakachukua tahadhari kwa kuvaa viatu. Lakini pia waepuke kukanyaga maji ovyo kwani ni hatari sana endapo utakuta nyaya imekatika na kugusa maji kwani umeme huwa na tabia ya kutembea na maji," alisema.

Mkaka alitoa wito kwa wananchi kuchukua tahadhari kubwa pindi panapotokea tatizo lolote linalohusu umeme na kuwataka kutogusa nyaya watakazoona ziko chini na badala yake watoe taarifa ofisi za Tanesco ili kuepuka madhara ikiwamo vifo.

Naye Ofisa Uhusiano wa shirika hilo Mkoa wa Kilimanjaro, Samuel Mandari, aliwataka wananchi kuepuka kufanya biashara au kilimo chini ya miundombinu ya umeme kwa kuwa ni hatari kwa maisha yao.

Mandari alisema shirika hilo halipendi kuona wananchi wakiathirika kutokana na umeme na kuwataka kuwa wazalendo kwa kuepuka kufanya shughuli zozote za kijamii chini ya miundombinu ya umeme.

## Wenye ulemavu, wazee 300 wapimwa magonjwa

**Na Paul William,** MOSHI

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Anderson Memorial Rehabilitation and Care Organization (AMRCO) limeendesha programu maalumu ya kliniki kwa wazee wasiojiweza na watu wenye ulemavu kwa ajili ya vipimo vya magonjwa yasiyoambukiza.

Kliniki hiyo imeendeshwa kwa siku mbili hivi karibuni katika eneo la Longuo B Manispaa ya Moshi na Mwika Wilaya ya Moshi ambako zaidi ya wazee na wenye ulemavu 300 walinufaika na kliniki hiyo.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Grace Saria, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa vipimo vilivyotolewa kwa makundi hayo ni pamoja na magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu na magonjwa ya kinywa na meno.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, lengo la kutolewa kwa vipimo hivyo bure ni kuwawezesha watu wasio na uwezo wakiwamo wazee na walemavu kupatiwa huduma hiyo muhimu.

Shirika hilo lilianzishwa mwaka jana likiwa na lengo la kuwahudumia wazee na watu wenye ulemavu ikiwamo kuwatembelea kwenye makazi yao na kuainisha changamoto zinazowakabili.

Saria alisema wazee wengi wanaishi na kutunzwa na vijana kutokana na watoto wao kukimbilia mjini kutafuta maisha, hivyo vijana hao kutokuwa na stadi za namna ya kuwatunza hatua ambayo imewafanya kujitosa kuwapa vijana hao stadi za namna ya kuwatunza wazee hao.

"AMRCO iliona hilo pengo kwa hiyo tunashirikiana na baadhi ya watumishi wa kanisa na tunataka Parish Worker akienda kumpa chakula cha bwana huyo mzee, amwangalie kwa undani na tunashirikiana pia na manesi na madaktari wastaafu walioko huko vijijini," alisema.

Alitoa wito kwa watu wanaoishi na wazee wasiojiweza pamoja na watu wenye ulemavu kutowaficha na badala yake wawe wakiwasaidia kuwapeleka kwenye maeneo husika, ili wapatiwe vipimo ili kubaini changamoto za kiafya zinazowakabili.

Kliniki ya kwanza ilifanyika kwenye ofisi za shirika hilo zilizopo kata ya Longuo B Manispaa ya Moshi, huku kliniki ya pili ikifanyika kwenye Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Mwika Mrimbo Uuwo, Dayosisi ya Kaskazini.

Mmoja wa madaktari walioshiriki katika kliniki hiyo, Mrosso Leonard, alisema kumekuwapo na changamoto nyingi kwa wagonjwa wa kisukari kusitisha matumizi ya dawa hatua ambayo imekuwa ikiwasabishia baadhi yao matatizo zaidi ya kiafya.






Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, jijini humo jana, kuhusu kongamano la kutangaza fursa za vivutio vilivyopo mkoani humo, linalotarajiwa kufanyika mwisho wa mwezi huu. Kushoto ni Katibu Tawala wa mkoa huo, Kessy Maduka. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Dodoma waandaa kongamano la kuvutia wawekezaji

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

MKOA wa Dodoma unatarajia kufanya kongamano la kwanza lenye lengo la kutangaza fursa na vivutio vya uwekezaji vilivyopo mkoani humo kwa wawekezaji mbalimbali wa ndani na nje ya nchi.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, wakati alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kongamano hilo litakalofanyika Juni 27 hadi 28, mwaka huu.

"Kauli mbiu ya kongamano hili itaongozwa na kauli mbiu ya 'Dodoma fursa mpya kwa uchumi wa Tanzania, wekeza Dodoma ikufanikishe," alisema.

Alibanisha kuwa zaidi ya watu 400 wanatarajiwa kushiriki kongamano hilo litakalofanyika ukumbi wa Jakaya Kikwete.

Alivitaja baadhi ya vivutio vya uwekezaji vilivyopo mkoani hapa kuwa ni Hifadhi ya Taifa ya Swagaswaga iliyopo wilayani Chemba, kilimo cha zabibu, mapango ya kale ya Kondoa, mifugo na kilimo.

Aliongeza kuwa mkoa umeandaa utaratibu mzuri na usalama wa kutosha kwa wawekezaji watakaohitaji kuwekeza katika mkoa huo.

"Katika hili pia tumejipanga vizuri ili kuhakikisha mwekezaji anapatiwa ushirikiano wa kutosha kupata ardhi katika eneo analohitaji kuwekeza na kwa muda mfupi, ili kufanikishiwa malengo ya uwekezaji," alisema.

Aidha, alisema Mkoa umetenga eneo la ardhi yenye ukubwa hekta 12,090 kwa ajili ya uwekezaji katika wilaya zote.

Aliwataka pia wajasiriamali wengine wa ndani na nje ya mkoa huo kujitokeza ili kuweza kutangaza bidhaa zao wanazozalisha.

# Bahi walilia elimu vitambulisho vya wajasiriamali

**Na Peter Mkwavila,**
BAHI

WAJASIRIAMALI wilayani Bahi wameiomba serikali kuwapa elimu kuhusu vitambulisho vya ujasiriamali vinavyotumika nchi nzima, ili waweze kuvichangamkia.

Ombi hilo lilitolewa jana baada ya Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana (UVCCM), Wilaya ya Bahi, Hassan Kadoke, kuwahimiza na kuwataka wajasiriamali hao kutovikwepa vitambulisho hivyo vilivyotolewa na Rais John Magufuli, kwa ajili ya kuwawezesha kufanya biashara zao kwa uhuru na bila kubugudhiwa.

Mmoja wa wakazi wa wilaya hiyo, Hadija Bakari, alisema wajasiriamali walio wengi hawana elimu, hivyo wanahitaji kupatiwa ili waweze kujitokeza na kuvinunua kwani hivi sasa wengi wanavikwepa.

"Wajasiriamali walio wengi wanashindwa kujitokeza kuvinunua kutokana na kukosa elimu zaidi, hivyo tunaiomba serikali kutoa elimu zaidi itakayowahamasisha wavinunue," alisema.

Naye Mwenyekiti wa UVCCM Bahi, Kadoke, aliwataka wajasiriamali kuvichangamkia vitambulisho hivyo kutokana na kuwa na faida kubwa kwenye biashara wanazozifanya.

Alizitaja baadhi ya faida hizo ni pamoja na kufanya biashara zao bila kubugudhiwa na kwamba pia watafaidika na kutambuliwa kwa kupitia vitambulisho hivyo ambavyo ni muhimu.

"Nina waomba wajasiriamali pamoja na hitaji lenu la kuomba elimu nawaomba mjitokeze kuvinunua vitambulisho hivyo ambavyo vitakuwa mkifanya biashara zenu kwa uhuru zaidi," alisema.

Aliwahimiza vijana kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi wa serikali za mitaa ambao utakaofanyika nchi mzima Oktoba mwaka huu.

# Wanafunzi wafurahia ziara ya mafunzo bungeni

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WANAFUNZI 120 wa Shule ya St. Anne Marie Academy na Brilliant za jijini Dar es Salaam, wameelezea namna walivyonufaika na ziara ya kimafunzo bungeni mkoani Dodoma hivi karibuni na kuomba utaratibu huo uwe wa kudumu.

Wanafunzi hao ni wale waliopata daraja la kwanza na la pili kwenye matokeo ya mitihani ya kidato cha nne mwaka 2018 kwenye shule hizo za Dar es Salaam.

Shule ya St Anne Marie ilikuwa ya sita kitaifa kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka 2018, ya kwanza Mkoa wa Dar es salaam na ya kwanza Wilaya ya Ubungo.

Kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka 2017 ilikuwa ya nane kitaifa, ya pili kwa Mkoa wa Dar es Salaam na ya kwanza Wilaya ya Ubungo.

Akizungumza na gazeti hili, mmoja wa wanafunzi hao, Jackline Malavanu, alisema hiyo ni mara yake ya kwanza kutembelea Bunge, hivyo amejifunza mambo mengi kuhusu mhimili huo.

"Tulipewa elimu kuhusu Bunge linavyoendeshwa, wabunge wanavyochangia mijadala na namna serikali inavyojibu hoja za wabunge, kwetu sisi ni faida kubwa sana na napongeza uongozi wa shule kwa kutupa fursa hii," alisema.

Mwanafunzi mwingine, Emmanuel Kimario, alisema shule mbalimbali zinapaswa kuiga mfano wa uongozi wa shule hiyo kwani ziara kama hizo zinawafumbua macho wanafunzi.

Alisema kupitia ziara hiyo wanafunzi wa shule hiyo wamejifunza masuala mbalimbali kuhusu uongozi na namna Bunge linavyojiendesha, hivyo aliomba isiwe mwisho kwani wamepata manufaa makubwa.

"Kwetu sisi hi ziara haitatutoka vichwani mwetu kwani tumejifunza na kujua mambo mengi ambayo yatatusaidia kitaaluma, tunaishukuru shule kwa kutupa fursa hii na tunaomba utaratibu huu uendelee," alisema.

Alisema mbali na kuwapeleka bungeni, shule hiyo imekuwa ikiwapeleka wanafunzi wa shule hiyo mbuga za wanyama kama Mikumi, Serengeti na Ngorongoro ambako wanajifunza masuala mbalimbali.

Abdulkarim Mawenge alishukuru shule hiyo kwa kutimiza ahadi yake ya kuwapeleka ziara ya mafunzo bungeni licha ya wanafunzi hao kutawanyika mikoa mbalimbali baada ya kuhitimu masomo yao ya kidato cha nne.


"Kwa kweli tunamshukuru Mkurugenzi wetu Jasson Rweikiza kwasababu ni mtu ambaye akiahidi ameahidi, wengi tulikuwa mbali na Dar es Salaam, lakini tumeitwa na wametupeleka bungeni kama walivyoahidi ni jambo kubwa sana kwetu wanafunzi," alisema.

Akizungumzia ziara hiyo ya kimasomo ya wanafunzi hao, Mkuu wa shule hiyo, Gladius Ndyetabura, alisema kuwa wanafunzi hao wamepewa ziara hiyo kama motisha kutokana na kufanya vizuri sana kwenye mitihani yao.

Alisema wanafunzi waliopata fursa hiyo ni wanafunzi 29 wa St.Anne Marie waliopata daraja la kwanza na 59 waliopata daraja la pili na sita wa shule ya Briliant waliopata daraja la kwanza na 20 waliopata daraja la pili.

Ndyetabura alisema imekuwa kawaida kwa shule hiyo kuwapa motisha wanafunzi wa shule hizo na ndiyo sababu shule imekuwa ikipata matokeo mazuri kwenye mitihani mbalimbali ya kitaifa.

Alisema wanatarajia kuanza kuwapeleka nchini Dubai, Uingereza hadi Marekani wanafunzi watakaokuwa wanafanya vizuri kwenye mitihani yao, ili iwe chachu kwa wengine kufanya vyema kwenye mitihani ya ndani na ile ya kitaifa.





# Dawa za kupunguza uraibu zasaidia vijana

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema kuwa utumiaji wa dawa za kupunguza uraibu 'Methadone' umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kusaidia vijana kuacha dawa za kulevya na kurudi katika familia zao.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Afya, Hamad Rashid Mohammed, katika kikao cha Bajeti cha Baraza la Wawakilishi, kinachoendelea visiwani hapa wakati akitoa ufafanuzi kuhusu matumizi ya dawa aina ya 'Methadone' ambayo hutumiwa kwa watu wenye nia ya kuachana na matumizi ya dawa za kulevya hatua kwa hatua.

"Dawa za kupunguza uraibu kwa vijana wanaotumia dawa za kulevya 'Methadone' zimesaidia kwa kiasi kikubwa watumiaji wake kuacha dawa hizo na kurudi katika familia zao," alisema.

Alisema vijana walioachana na dawa za kulevya sasa wamerudi katika familia zao na kupokelewa, huku wakiaminiwa na wengine kurudi katika ajira za serikali. Aidha, alisema hadi kufikia Machi 2019, jumla ya vijana wapya 282 wamesajiliwa na kupatiwa dawa za kupunguza uraibu na utegemezi wa dawa za kulevya wakiwamo wanawake 43, huku vijana 621 wanaendelea kutumia dawa hiyo ambayo ndiyo inayotumika kwa ajili ya vijana kuacha dawa za kulevya hatua kwa hatua.

"Mheshimiwa Spika nataka kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba dawa ya 'Methadone' ambayo ndiyo inayotumiwa kwa ajili ya vijana kuachana na dawa za kulevya imeleta mafanikio makubwa, huku vijana 20 wakiacha kutumia dawa hizo moja kwa moja," alisema.

Aidha, aliwaambia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Ukimwi bado upo, huku ukiendelea kuziathiri familia za wananchi wa Unguja na Pemba na wizara yake inatekeleza mwongozo wa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), ikiwamo sera ya kufikia shabaha ya 90,90, ifikapo mwaka 2020, ikiwamo asilimia 90 ya kujitambua na asilimia 90 ya kusajiliwa na wameanza matibabu ya kupunguza makali ya VVU. Alisema hadi kufikia Machi 2019, watu 196,289 walichunguzwa na kupimwa afya na kati ya hao watu 1,376 sawa na asilimia 0.7 waligunduliwa na virusi vya Ukimwi.



Jopo la majaji saba wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2018, chini ya Mwenyekiti wake, Kiondo Mshana (katikati), likipitia sehemu za kazi 644, zilizowasilishwa na waandishi wa habari nchini, kwa ajili ya kushindanishwa katika tuzo hizo, mjini Bagamoyo, mkoa wa Pwani jana, ambapo zoezi hilo, litachukua siku saba kuanzia Juni 13 hadi 19, 2019. Majaji wengine katika jopo hilo ni Selemani Mpochi, Hassan Mhelela, Joyce Bazira, Pudenciana Temba, Aisha Dachi na James Gayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana vyuo vikuu wahamasishwa kazi za kujitolea

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VIJANA wanaosoma katika vyuo vikuu nchini wametakiwa kuchangamkia fursa za kufanyakazi kwa kujitolea zinazotolewa na Umoja wa Kimataifa wawapo vyuoni na nje ya vyuo.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Mradi wa Kujitolea wa Umoja wa Kimataifa UN Volunteers, alipokuwa akizungumza na wanafunzi wa vyuo vikuu vya SUZA, ZU na IPA kwa nyakati tofauti jana.

Alisema, fursa ya kujitolea zinazotolewa na UN zina faida kwa vijana hao kutokana na kupata uzoefu ambao utawajengea uwezo wa kufanya kazi kwa kujitolea bila ya kuhimiza maslahi mbele.

Alisema kuwa mradi huo wa kujitolea unalenga vijana wasomi ambao bado wanaendelea na masomo yao katika vyuo vikuu kwa vijana wa umri wa miaka 18-29.

Hata hivyo, alisema mradi huo umeanzishwa ili kuandaa dhana ya uzalendo kwa kujitolea ambayo inakuwa ni moja ya chachu kubwa ya kuleta maendeleo katika nchini.

Sambamba na hilo alieleza kuwa katika mradi huo wamewapa vipao mbele sana vijana hao wasomi kutokana na kwamba wana mawazo mapya ya kuleta chachu ya maendeleo kwa nchi yake.

Hivyo alisema kuwa utekelezaji wa shughuli za maendeleo ndio utakaowapa fursa ya shughuli za maendeleo.

# ZECO yasambaza umeme vijiji 46 Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la Umeme Zanzibar (ZECO), limefanikiwa kusambaza nishati ya umeme vijijini kwa kiwango kikubwa, jumla ya vijiji 46 vimepatiwa nishati hiyo na hivyo kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati, Salama Aboud Talib, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019-2020, huko Chukwani katika kikao cha bajeti kinachopendelea.

Alisema hatua hiyo imefanyika kuwanufaisha wananchi wa visiwa hivi ikiwa pia ni pamoja na kwenda sambamba na ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2015-2020. Alisema kazi ya usambazaji wa umeme katika visiwa vidogo viliopo Unguja na Pemba, imefanikiwa na wananchi kunufaika na nishati hiyo na kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi.

Alivitaja visiwa ambavyo tayari wananchi wake wananufaika na nishati ya umeme ni pamoja na Kojani, Uvinje, Kisiwa Panza pamoja na Makoongwe kwa upande wa Pemba, huku kisiwa cha Tumbatu wananchi wake wakitumia nishati hiyo kwa Unguja.

"Mheshimiwa Naibu Spika napenda kuliarifu Baraza la Wawakilishi kwamba tumepiga hatua kubwa katika usambazaji nishati ya umeme vijijini pamoja na visiwa vidogo vilivyopo Unguja na Pemba na hivyo kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na maendeleo," alisema.

Hata hivyo, alisema katika usambazaji huo Shirika la Umeme limetumia jumla ya Sh. bilioni 2.2 ikiwamo kununua vifaa na kulipa fidia kwa wananchi walioharibiwa mazao ya kilimo.

Mapema waziri huyo alisema kuwa Mamlaka ya Majisafi na Salama (ZAWA) inakusudia kutekeleza miradi mitano ambayo itasaidia kuimarisha huduma za majisafi na salama ikiwamo vijijini na kukiri kuwapo kwa matukio ya uvamizi wa vyanzo vya maji vilivyopo Unguja na Pemba na hivyo kutishia uzalishaji wa nishati hiyo.

Aliitaja miradi hiyo ukiwamo wa upatikanaji maji Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, mradi wa ujenzi wa visima vya kuzalishaji maji kutoka China pamoja na mradi wa usafi wa mazingira kutoka India, wa kuimarisha visima vya maji na kuviunganisha na umeme wa Rasilkhema, pamoja na wa kulinda vianzio vya majisafi na salama.

Katika hotuba yake hiyo Waziri Aboud aliwaomba wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuidhinisha jumla ya Sh. bilioni 156, kwa kazi za kawaida na maendeleo pamoja na utekelezaji wa miradi ya majisafi na salama na nishati ya umeme.



Soma UK. 16

**JUX**

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI JUNI 15, 2019



# 'NENDA KILIONI'

## WASANII KUVUNJA BENKI KUNUNUA MAWIGI

UK.15

BASI SAWA



## Jeniffer anapohubiri 'Sema Kweli' mbele ya Mungu

MWIMBAJI wa nyimbo za Injili, Jeniffer Mgendi, ameachia singo yake inayoitwa 'Sema Kweli' ambayo imeanza kutamba kwa kasi.
Akizungumza hivi karibuni, Jeniffer, amesema wimbo huo ambao aliutambulisha rasmi juzi umepata mafanikio baada ya mashabiki kuupokea vizuri.
"Wimbo wangu huu 'Sema kweli' nataka kuwaambia watu kuwa wanyenyekevu mbele ya Mungu pamoja na kusema kweli kwa kila kitu kinachomtokea," amesema Jeniffer.



## Dully ubaba na Harmonize umetoka wapi?

MWANAMUZIKI mkongwe wa Bongofleva, Dully Sykes, amesema msanii mwenzake Harmonize anamchukulia kama mtoto kutokana na heshima anayompa.
Dully amesema kutokana na uhusiano wake huo imekuwa rahisi kufanya kazi pamoja na kutoa ngoma kali zinazopendwa na mashabiki.
"Nadhani kutokana na heshima yangu kwa kila mmoja wasanii wengi wananipenda na hata Harmonize ananiheshimu. Sipendi kugombana na wenzangu wala kuingia katika mabifu ambayo mimi hayanihusu," amesema Dully.



# UONGO!
# Queen Darleen atamba

MWANADADA anayetamba katika muziki wa Bongofleva, Queen Darleen, amesema huwa hajali maneno ya uongo yanayozungumzwa na watu, badala yake anaangalia kwa kiasi gani anaingiza pesa.
Akizungumza hivi karibuni, Queen Darleen, amesema watu wanamuhusisha na mambo ya mapenzi ya jinsia moja, lakini kwake anajiamini kuwa ni mwanamke kamili mwenye hisia za kike.
"Unajua unapokuwa na jina kubwa kila mtu atasema lake na kutaka kujua mambo yako ya ndani, kiujumla mimi siangalii watu wanavyosema ninachoweka mbele ni jinsi gani nitanyanyua kazi yangu na kujiingizia kipato," amesema.

## INSTA-TWITTER





**Asitokee** binadamu yeyote yule akakukatisha tamaa katika ndoto zako-**Hamisa Mobeto.**



**Unaweza** kufurahia maisha yako kama utaamua kuwa wewe - **Madee Ali.**



## Timbulo amshukuru Jux kubadilika

MKALI wa muziki wa Bongofleva, Timbulo, amesema kumshirikisha Jux katika wimbo wake mpya halikuwa jambo la bahati mbaya.

Akizungumza na BT jana Timbulo amesema katika singo hiyo 'Nashukuru' Jux ameonekana kuitendea haki kutokana na uimbaji ambao umebadilika kwa kiwango kikubwa.

"Nakumbuka sikuwa na kazi kubwa kuingiza sauti ya Jux katika wimbo wangu, kwangu namuona ni mwanamuziki mwenye kipaji na anayebadilika kutokana na aina ya muziki anaotakiwa kuimba," amesema Timbulo.




@burudanitele

**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**



# 'NENDA KILIONI'
## Wasanii kuvunja benki kununua mawigi

ONGEZEKO la kodi kwa nywele za bandia la asilimia 10 kwa zile zinazozalishwa ndani na asilimia 25 kwa zinazotoka nje, itawafanya idadi kubwa ya wasanii wa kike kuvunja benki zao kugharamikia urembo huo.

Pendekezo hilo limetolewa na Waziri wa Fedha na Mipango, Philip Mpango, wakati akiwasilisha Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Idadi kubwa ya wasanii wa muziki na filamu wanatumia nywele za bandi wakati wakiwa katika shughuli zao pamoja na matembezi ya kawaida.

Warembo wanaotajwa kuathiriwa na matumizi ya nywele za bandia ni Wema Sepetu, Irene Uwoya, Aunt Ezekiel, Lulu, Flora Mvungi, Riyama Ally na Shamsa Ford.

Kwa upande wa wasanii wa muziki Maua Sama, Linah, Nandy, Vanessa Mdee na wengine kibao.



Pamoja na nywele za aina hiyo kuwapa mvuto wa kipekee, lakini iliwabidi kutumia pesa nyingi kuzinunua kutokana na aina na kampuni iliyozitengeneza.

Kutokana na mapendekezo hayo ya serikali, sasa wasanii watatakiwa kuangalia upya bajeti zao na wakati mwingine kufikiria njia ya utunzaji wa nywele za kiasili kama kusuka nywele au kuzipunguza ili kuepuka matumizi makubwa.

Wakati anasoma makadirio ya bajeti Waziri Mpango alisababisha Bunge kulipuka kwa kelele kwa wabunge wakipiga meza zao wakionyesha kufurahia pendekezo hilo.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Mganga** wa timu nishafuzu. Dua zote hapa Dubai kwa Waarabu wenzangu. Niwahakikishie tu AFCON tutashinda mechi zote, ila mnakumbuka lakini mashar-ti yetu? Msije kusema mganga kala pesa za bure - **Mkude Simba.**



**Asante** kwa kunipenda. Asante kwa kunifungua macho. Asante kwa kunifanya nione thamani yangu. Kuna muda nilijipoteza kabisa ila umekuja kunionesha njia, sikujua kama ningeweza kupenda tena katika namna hii, haikuwa rahisi. Endelea kunishika mkono Baby, nitakupenda sana, wewe ni mwanaume sahihi kwangu - **Aunt Ezekiel.**



**Kamwe** usiruhusu mtu asiye na msaada kwako aichoshe akili yako - **Johari.**

# Kuumbe!



# JUX

## HANA SHIDA, MPE TU UTAMPENDA

**Na Adam Fungamwango**

'NASHUKURU ' ni wimbo mpya wa Timbulo ambao hauna hata wiki tangu utambulishwe rasmi.

Ngoma hii imerushwa kwenye mtandao wa Instagram rasmi Juni 11 na kwa muda mfupi tu umeanza kujizolea umaarufu na mashabiki wengi kuuangalia.

Mpaka Ijumaa, tayari ulikuwa umeshaangaliwa na watu 207,074. Katika ngoma hii, Timbulo amemshirikisha msanii Jux.

Achana na maudhui ya wimbo, achana na Timbulo jinsi alivyoimba kwa kulalamika kama ilivyo kawaida yake, kikubwa kilichowashangaza na kuwafurahisha wengi ni jinsi msanii Jux alivyoimba kwenye ngoma hii.

Kwa kawaida, wengi wamemzoea Jux kuimba nyimbo za R&B ambazo ni za kimapenzi za taratibu na kubembeleza. Lakini sasa wala siyo hivyo tena.

Jux ameonyesha kukomaa kimuziki. Amebadilika kabisa na kupamba na Timbulo kwenye uimbaji.

Beti ya mwanzo aliimba mwenyewe Timbulo, lakini beti ya mwisho imeimbwa na Jux na kwenda na spidi ile ile kiasi cha anayesikiliza kwenye redio na si kuangalia kwenye TV anaweza kudhani bado Timbulo anatiririka.

Jux ameimba kwa staili ya bongo fleva asilia kama ambavyo wanafanya wasanii wengi kwa sasa kama kina Ali Kiba, Aslay, Timbulo, Rayvanny, Harmonize na wengineo.

Vyovyote itakavyokuwa, kama msanii huyo alilazimishwa kuimba hivyo kutokana na matakwa ya wimbo wenyewe, lakini imeonyesha kuwa ni mwanzo mzuri kwake kwani anaweza kutunga wimbo wowote mpya na kuimba kwa staili hiyo.

Kwa kawaida mwanamuziki au msanii anatakiwa kujifunza kila siku na kubadilika na kuimba nyimbo za aina mbalimbali badala ya kung'ang'ania kuimba kwa staili moja.

Msanii au mwanamuziki wa aina hiyo mara nyingi hupitwa na wakati, lakini mwenye kubadilika naye hubadilika kulingana na wakati.

Mfano mwanamuziki wa Congo JB Mpiana, wengi wanamfahamu kwa kuimba nyimbo za staili ya 'Ndombolo' zenye mapigo ya kasi.

Lakini huyo huyo ni mtaalamu na ana uwezo mkubwa wa kuimba nyimbo za taratibu na amefanya hivyo kwenye nyimbo kama 'Omba', 'Ilove You', na nyingine nyingi na kama ukimsikiliza kwenye nyimbo huzo, huwezi kudhani kama ni JB Mpiana yule unayemfahamu.

Kwa sasa Jux hakai sehemu moja, unaweza ukasikia ngoma yake kwa staili ya R&B, lakini pia ukamsikia akikamua kwa staili ile ya kibongo fleva halisi.

Hili ni somo hata kwa wale wasanii wa Hip-hop au marapa, si kama waache kuimba kwa staili hiyo, ila wajaribu kujiongeza, wanaweza kubadilika kuimba kwa staili mbalimbali ili kujiongezea mashabiki, umaarufu, lakini pia muziki wao kutopitwa na wakati.

# WALIOANZA WADOGO, WAKAPASUA UKUBWANI

**Na Adam Fungamwango**

MWANZONI mwa miaka ya 2000 ndipo muziki wa bongo fleva ulipoanza kuchipua nchini Tanzania na miaka ilivyozidi kwenda mbele wasanii wengi walipoanza kuukubali.

Ni muziki ambao haukukubalika kirahisi, kwani katikati ya miaka ya '90 ulionekana kama ni muziki wa kihuni, lakini walipoingia baadhi ya wasanii na kufanya mapinduzi makubwa kwa kutunga ujumbe wenye maadili, wakiongozwa na Joseph Haule maarufu kama Profesa Jay, zamani akiitwa Niger J, sasa ni Mbunge wa Jimbo la Mikumi, hata watu wazima walianza kuukubali muziki huo.

Wazazi nao walianza taratibu kuwaruhusu vijana wao kujiingiza kwenye muziki huo.

Ndiyo maana mbali na wasanii wengi ambao walikuwa vijana kuanza kuimba bongo fleva, kuna wasanii walioingia kwenye gemu hili wakiwa na umri mdogo sana.

Umri wao uliwafanya kupachikwa au kujipa majina mbalimbali yakiashiria utoto wao wakati huo.

Hawa ni baadhi ya wasanii ambao walianza kuingia kwenye muziki wa kizazi kipya wakiwa na umri mdogo, ingawa kwa sasa wameshakuwa watu wazima.

**Dogo Ditto**

Kwa sasa anajulikana kama Lameck Ditto. Ngoma yake inayotamba au iliyotamba kwa miaka ya karibuni na kumtambulisha sana ni 'Moyo Sukuma Damu'. Huyu ni msanii wa siku nyingi wa bongo fleva aliyeanzia utoto. Kwenye miaka ya kati hakusikika, labda alikuwa kwenye mishemishe zingine.

Akiwa na umri mdogo kabisa, aliibuliwa kipaji chake na rapa mkongwe ambaye alikuwa kwenye kiwango cha juu wakati huo, Afande Sele mwaka 2003.

Baada ya hapo alishirikishwa kwenye ngoma zote za Afande Sele, kabla ya kusimama mwenyewe na kutambulika kwenye ulimwengu wa sanaa, akipachikwa jina la Dogo Ditto. Ukimuona kwa sasa huwezi kuamini kuwa ndiyo Dogo Ditto yule.

**Mr Blue**

Jina lake kamili ni Kheri Sameer Rajab, lakini kisanii anajulikana kama Mr Blue. Akiwa hajavuka hata umri wa miaka 18 tayari alishakuwa staa nchini Tanzania kwa ngoma yake ya 'Mr Blue' iliyompa hata jina hilo, lakini katika kuonyesha kuwa hakubahatisha akatoa ngoma nyingine akaaiita 'Mapozi'. Hiyo ilikuwa ni katikati ya miaka ya 2000. Baadaye alipotea kwenye ulimwengu wa muziki, lakini ameibuka tena kwenye miaka ya karibuni na ngoma kama 'Blue' akimshirikisha Nandy, 'Hatufanani', akiwa na Shetta na Juz na 'Waombe Po' akimshirikisha Rayvanny. Muonekano wake ni tofauti na ule wa mwanzo alipokuwa bado 'kinda'.

**Dogo Janja**

Msanii wa muziki wa kizazi kipya kwenye miondoko ya hip hop, alikuwa kijana mdogo katikati ya miaka ya 2000, akitoka na ngoma ya 'Anajua' akishirikiana na Madee.

Huyu si mwingine bali ni Abdulaziz Abubakar. Ngoma hiyo iliwachengua wengi na mashabiki wakampachika jina la Dogo Janja.

Madee ndiye aliyevumbua kipaji hiki. Baada ya hapo alisimama mwenyewe na kutoa ngoma mbalimbali hadi hii leo. Kwa sasa amekuwa mkubwa, ingawa mwili wake bado haujabadilika sana. Na bado anajiita Dogo Janja.

**Dogo Aslay**

Nyota ya Aslay ilianza pale alipoonekana kwenye tamasha la Zanzibar akiimba 'laivu' wimbo wa Majiraji Rajabu ulitwao 'Siwema.'

Kuna watu wakaona ni madini inayotembea. Haraka alipofika Dar wakamuingiza studio na kutoa ngoma iitwayo 'Nitakusema'. Hii ndiyo ngoma iliyomtoa kutoka kusikojulikana hadi kuwa staa mkubwa akiwa na umri mdogo, kiasi cha kuchukuliwa kwenye kundi la 'Yamoto Band'.

Wakati huo wote mashabiki wake walikuwa wakimwita Dogo Aslay. Kutokana na sasa kuwa na umri mkubwa wa ujana, anajulikana kama Aslay Isihaka.

**Nandy**

Ni msanii ambaye nyota yake imeanza kung'aa akiwa na umri mdogo sana, hivyo kama atajitunza na kulinda kipaji chake anaweza kufanya muziki kwa miaka mingi ijayo kwa sababu bado umri unamruhusu.

Kwa miaka miwili amekuwa moto wa kuotea mbali alitoa ngoma ambazo zimekuwa zikiwaacha hoi mashabiki wake.



# Vijimambo

1. Hii ndio inaitwa 'nikinywa maji, nakuona kwenye glasi' - Agatha Mbale, Moro Town.
2. Ai weeewe, naoomba - Ebby Mbwambo, Tanga.
3. Hahahaaa, endelea kuomba tu mzee baba, atakupa tu - Maunda Alawi,
4. Duuh, kweli utoto kazi! Kidume kinategemea kabisa kimegewe mkate! - Beneali Moussa, Zenji.
5. Naomba, ukinipa na mie nikinunuliwa soda nakupa - Mauwa Minde, Kibada Kigamboni DSM.
6. Lazima huyo dogo atakua wa Bush Stars, anaiomba picha mkate! - Sultani Ubwa, Kibada DSM.
7. Endelea tu kuomba, huyo siyo mchoyo atakumegea tu - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
8. Kama ulikuwa hujui tafsiri halisi ya neno 'zwazwa', basi ndio hiyo - Beneali Moussa, Migombani Zenji.
9. Naenda kukusemea kwa mama yako umeomba mkate kwa watu ->Julius Anthony, Usagara Tanga.
10. Acha uchoyo wewe, mwenzio anakuomba ndio unaingiza wote mdomo! - Mama Nah, Manzese DSM.
11. Mwache na uchoyo wake, na wewe ukinunua vitu vyako usimpe - Rehema Bwahoja, Buguruni DSM.
12. Dogo utachubuka 'makongoro' kwa kupiga magoti, hiyo picha tuu - Subira Bwahoja, DSM.
13. Jamani, si mngemuambia kama hiyo ni picha tu sio mtu kweli. Ona sasa anavyotia huruma - Dule DSM.
14. Yes, hiyo ndio dawa ya ombaomba. Kesho leteni roli lenye picha ya hela - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
15. Daaah, mjukuu wa 'Matonya' anadhalilika hivi hivi kwa picha tu - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
16. Huyo naye kubwa zima hajajua tu picha na mtu wa ukweli? Muacha achune magoti - Kole, Msata Pwani.
17. Hapo atalifuata gari mpaka wapi kwa kupiga magoti hivyo Magdalena Kachenja, Mabwepande DSM.
18. Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba - Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.
19. Kweli walimu wanakazi. Huyo mpaka aje kujua hiyo ni picha tu si atakua Chuo Kikuu! - Pili Mpanjira DSM.
20. Mmmh, mie mgeni hapa, acha nipite tu! - Abass Ngulunga, Msasani Macho, DSM.
21. We mtoto utagongwa na magari buree. Huyo sio mtu kweli ni picha tu - Bernad Isuja, Makore Dodoma.

**SMS Bomba ya Leo:**

**Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba -Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.**

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0682 808 694**



# Changudoa Mkaa unapogeuka dhahabu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine binadamu anapitia kwenye mazingira magumu na tata hadi anapofikia umri wa utu uzima.

Kwa wale wanaokwenda kwenye makanisa, ni mashuhuda kwa watu wanaotoa ushuhuda kuwa alikuwa wachawi, majambazi, au wala rushwa, lakini baadaye wanatubu, wanamrudia Mungu na kuwa watu wema.

Kwa maana halisi hata mkaa unaweza kuwa dhahabu kama ukiuthamini na kuutumia vizuri.

Hiki ndicho kisa kilichomo kwenye filamu hii itwayo 'Changudoa.'

Filamu hii imechezwa na wasanii kina Nassor Ndambwe, Flora Mvungi, Abdul Mhema na wengine wengi.

Inaanza kwa kumuonyesha kuwa Flora ni msichana ambaye kazi yake ni kuuza mwili.

Anafanya kazi ya ukahaba, ndiyo inayomfanya kupata mahitaji yake ya kila siku.

Filamu inamuonyesha kuwa yupo na mteja kwenye nyumba ya kulala wageni.

Lakini anafanya kitu cha ajabu, baada ya kuamka huku mwenzake akiwa amelala na kwenda kumkomba kila kitu na kutimka, wakati mteja wake akiwa kwenye usingizi fofofo.

Anapoamka hamkuti mwenzake kitandani na anashangaa kuona nguo zake zimetupwa chini na hatimaye kugundua kuwa amelizwa kila kitu na changudoa aliyemchukua.

Upande mwingine anaonekana Flora yuko na shoga yake wakishauriana ni jinsi gani ya kwenda kutafuta mabuzi wa kuwachuna.

Mara anakuja Abdul na kumuomba Flora wawe pamoja usiku huo. Wakiwa kwenye nyumba ya kulala wageni anavamia mtu mmoja anayejulikana kwa jina la Ndambwe ambaye anatoa bastola kumuonyesha Flora na kumwambia amlipe pesa zake, sivyo atammaliza. Hili linamuogopesha Abdul na kuamua kuchukua yeye jukumu la kulipa pesa hizo.

Abdul anaokana kumpenda sana Flora kiasi cha kumuambia kuwa anahitaji kumuoa.

Kutokana na hilo, anaamua kumpeleka nyumbani kwake. Wanapofika wanakutaka na Ndambwe ambaye analianzisha vurugu.

Mwenye nyumba anatoka baada ya kuona nje kuna ugomvi, lakini anakutaka na mpangaji wake Abdul pamoja na Flora ambaye pia ameshawahi kumchukua na kwenda naye kufanya naye mapenzi gesti.

Sasa ugomvi unakuwa mkubwa zaidi kiasi cha Flora, kuwachoropoka na kutimua mbio kuepuka kupigwa.

Anapofika nyumbani anawapigia simu shoga zake kuwaeleza yaliyompata na jambo hilo lilimuathiri kisaikolojia kiasi cha kuamua kuachana na kazi hiyo.

Akaamua kufanya kazi ya kuuza maandazi, lakini kwa sababu hajaizoea, alijikuta sehemu kubwa ya maadazi akirudi nayo nyumbani na kuyatafuna yeye na shoga zake.

Alikaa na kufikiri, akili ikamtuma kurudia tena kazi yake ya uchangudoa. Huko tena alikutana na Abdul. Flora alitaka kukimbia akidhani atapigwa, lakini jamaa anamwambia hakuwa na nia hiyo, ila azma yake iko pale pale ya kumuoa.

Flora alikataa kwa madai hana hadhi hiyo, lakini Abdul alimbembeleza na kumwambia kuwa kitu anachotakiwa kufanya ni kuanza ukurasa mpya akishakuwa mke wa mtu.

Flora alitafakari kazi ya uchangudoa na kuona tayari imeshamletea matatizo, huku kazi ya kuuza maandazi ikiwa hailipi, upande wa pili kuna mtu anamtaka awe mkewe, kitu ambacho ni nadra sana.

Mwishowe anakubali kuolewa na anaamua kubadilika kitabia. Abdul amuoa na kumuondoa sehemu ambayo amezoeleka na kwenda kuishi naye mbali na hapo. Akawa mke mwema.



# HOLLYWOOD SI SHWARI

## PEPO WA KUACHANA ATAWALA KILA KONA

PENGINE jinamizi baya linaendelea kutembea katika mji wa mastaa wa Hollywood, baada ya nyota kadhaa wa filamu kuripotiwa kuachana katika kipindi cha miezi mitano pekee, sasa ni zamu ya Joe Budden na Cyn Santana, ambao imeelezwa wamepigana kibuti.

Kulingana na uvumi ulioenea katika jiji hilo lenye kila aina ya maraha chini Marekani, Joe na Cyn wameachana wakiwa muda mfupi tangu wavishane pete ya uchumba.

Taarifa zinaeleza kuwa kuna kila dalili kuwa wawili hao hawana tena uhusiano wa kimapenzi, japokuwa kuna ukimya umetawala kuhusu hali hiyo kwa kila mmoja kukataa kuzungumzia jambo hilo.

Tukio la kuachana kwa mastaa hao ni mfululizo wa matukio kadhaa ya kutengana na kupeana talaka kwa nyota wa Hollywood tangu kuanza kwa mwaka 2019.

Kulingana na mtandao wa Hollywood life, wapenzi hao walikuwa na mgogoro mkubwa kabla ya kuamua kila mmoja kuchukua njia yake.

Cyn Santana ameonekana akikatiza mitaa akiwa hana pete katika kidole chake cha mkononi jambo ambalo linaweka wazi kwamba yupo singo.

Wote Joe na Cyn kila mmoja amemuondoa mwenzake urafiki katika mitandao yao Instagram.

Katika kuonyesha hali si shwari tena, Cyn amefuta picha zote alizopiga akiwa na Joe kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Joe Budden and Cyn Santana walifunga uchumba kwa kuvishana pete Desemba 2018 mwaka jana.

Lakini hakuna uhakika kwa nini wapenzi hao wameamua kuvunja uhusiano wao bila ya kutoa taarifa yoyote.



# Jamani nyie waigizaji wa kike muwe makini

WAIGIZAJI wa kike chipukizi wameaswa kuanza kujenga uhusiano wa kimapenzi kabla hawajapata umaarufu ili kujilinda na taarifa za uzushi.

Ushauri huo umetolewa na msanii maarufu Ruth Kadiri, ambaye mesema uhusiano imara ni ule unatoka moyoni na si umaarufu wa mtu, hivyo ni muhimu kuwa na mpenzi kabla mtu hajapata umaarufu.

Ruth Kadiri amewataka wasichana wanaoingia katika tasnia ya filamu kuangalia jinsi wanavyopigana na wakati jambo ambalo linakuwa vigumu pale anapokuwa na jina kubwa kiasi ambacho ni vigumu kuwa na uhusiano wa kweli.



## Kumbe ndoa zingine balaa tupu

DADDY Freeze ambaye anatamba katika mitandao ya kijamii nchini Nigeria, amesema ndoa si jambo linaloleta furaha kama wanavyoamini wengi, badala yake inaweza kuleta majuto.

Ujumbe huo ambao aliweka katika mtandao wake wa kijamii ulifuatia na mjadala mrefu kuhusu wanawake kupata unyanyasaji dhidi ya wanaume katika nyumba zao.

Katika ujumbe huo alitoa mfano ndoa yake ya kwanza ambayo alitumaini angepata tulizo la moyo, badala yake ilikuwa kinyume na matarajio yake.

## Tonto arushwa roho kiaina

OLAKUNLE Churchill mume wa zamani wa mwigizaji wa Nollywood, Tonto Dikeh, ameamua kuvunja ukimya baada ya kumweka wazi kimwana wake mpya.

Churchhill alitumia mtandao wa Instagram kuweka picha za mrembo huyo na kumtakia heri ya siku yake ya kuzaliwa, huku ikiambatana na ujumbe mzito wa kimahaba.

Sehemu ya ujumbe wake ambao unaweza kumkosesha usingizi Tonto ulisema "Nafurahi kukuangalia ukiwa na mtu ambaye anakupa amani furaha ya siku yako ya kuzaliwa mpenzi wangu,"





## Wendy mambo ya ujana bado unayo?

UNAWEZA kusema kwamba anashindana na uzee, kwani msanii maarufu Wendy Williams, ameonekana bado yumo kwani siku chache baada ya kuachana na mume wake Kelvin Hunter, ameopoa kidume mwingine tena bado mbichi.

Katika kuonyesha kwamba yeye sio mzee kama watu wanavyosema, ametupia picha zake mpya akionekana akiwa na uso wake ukiwa hauna makunyazi sawa na binti wa miaka 20.

Kulingana na mtandao wa TMZ, Wendy ameonekana hivi karibuni na mwanaume huyo katika mitaa ya jiji la Los Angeles na inaelezwa wawili hao wamepanga kuhamia jumla katika mji huo kuishi pamoja.

## Khloe anapolia na Uber

ALIYEKUWA mshiriki wa shindano la Big Brother Nigeria, Khloe, amewashutumu madereva wa magari ya Uber nchini humo kutokuwa na tabia za kistarabu kwa wateja wao.

Akizungumza katika kipindi cha TV, Khloe, amesema alichofanyiwa na dereva mmoja wa magari hayo hatakisahau kwani alimchelewesha safari yake bila ya sababu ya msingi.

"Madereva wa Nigeria sijui wanapatikana vipi kupewa kazi, watu hawana ubinadamu na wamenivunja moyo kabisa," ameandika Khloe.



SAFU



## Mionzi ya Sheria

Na John Juma
0716217615

# Fahamu msingi na wajibu kwa kila raia kujua sheria za nchi

HAKUNA jamii duniani isiyo na taratibu au misingi ya namna ya kuishi na kufanya shughuli za kila siku.

Jamii yeyote isiyokuwa na utaratibu, basi migongano itakuwa ni sehemu ya maisha yao ya kila siku.

Hivyo lazima kuwe na utaratibu maalumu ambao jamii hii utaishi kwao, utaratibu huu utaongoza au utaathiri nyanja zote za maisha katika jamii hiyo. Utaathiri nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa na hata utamaduni wa eneo hilo. Hivyo tunaweza tukaita utaratibu huu sheria.

Tuangalie basi umuhimu wa mwananchi wa kawaida kufahamu sheria katika jamii, japo chache ni hizi zifuatazo;

Ibara za 12 hadi 29 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara) inaelezea juu ya Haki na Wajibu wa kila mwananchi.

Hivyo ni jukumu la kila mwananchi kusoma na kuzifahamu (vizuri) Sheria za Nchi: Zaidi sana, *Ibara ya 26(1)-(2)* ya katiba tajwa.

Hapo utafahamu mipaka ya kutumia uhuru na haki yako, hii ni kwa sababu hakuna haki isiyokuwa na wajibu/mipaka.

Kwa mfano, Ibara ya 18 ya Katiba ya nchi inatoa uhuru wa kujieleza na kutoa maoni, lakini kumewekwa mipaka ya kutumia uhuru huo katika Ibara ya 30 ya katiba ya nchi, kwamba haki na uhuru wowote ule usitumiwe kwa namna ya kuingilia na kuathiri uhuru na haki za watu wengine.

Utatambua kuwa ni wakati gani utahesabiwa kuwa na hatia. Si kila mtu anayefahamu kuwa ni wakati gani atakuwa na hatia. Ibara ya 13(6)(b), Katiba ya Jamhuri ya Muungano, 1977 (kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara) inaeleza kuwa "mtu yeyote aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai hatahesabika kuwa na hatia ya kosa mpaka pale itakapothibitika kuwa ametenda kosa hilo."

Kwa maana hiyo atakuwa na haki zote anazostahili mtu asiye na hatia mpaka pale itakapothibitika kuwa ana hatia ya kosa hilo.

Haya yote, mtu hatoyafahamu kama hana uelewa wa sheria au hapendi kusoma sheria au hataki kufahamu utaratibu wa kisheria. Mathalani, kwa mshtakiwa wa kosa la jinai hatofahamu haki zake za msingi, ikiwamo (ile) ya kuwakilishwa na kutetewa na wakili.

Kifungu cha 54(1) cha Sheria ya Mwenendo ya Makosa ya Jinai, Sura ya 20 (Criminal Procedure Act Cap. 20) inaonyesha kutambua Haki ya Mtuhumiwa kuruhusiwa au kupatiwa Utetezi/Msaada wa Kisheria (Legal Aid); sanjari na 2, 21(1)-(3), 22(a)-(c), 27(a)-(b) na 44(1)-(2) vifungu vyote vya Sheria mpya ya Msaada wa Kisheria, 2017.

Hii imekwenda mbali zaidi kwa kuruhusu fursa husika kwa mashauri yote, jinai na madai!

Kimsingi, mtu asiyejua haya hawezi kudai haki yake pale atakapokuwa chini ya mikono ya sheria. Ndiyo pale atakapolazimika kutoa rushwa au kufanya vitendo vingine visivyofaa kwa kuwa hajui utaratibu wa kufuata kisheria. Utajua utaratibu wa kupata haki yako pale inapodhulumiwa au inapoonekana kutaka kupokonywa na mamlaka za kiserikali au mamlaka zingine halali au mtu mwingine yeyote.

Utaishi kwa kujiamini, kwani kila jamii ina utaratibu maalumu. Watu wengi wameshindwa kuishi kwa kujiamini kwani kila wakati wanajihisi kuwa ni wenye hatia.

Wengi wanaishi bila kufuata utaratibu na hivyo kujijengea hofu kubwa. Ukifahamu sheria utaishi kwa kujiamini katika jamii yako kwani hutavunja utaratibu bali utafuata utaratibu mahususi wa kisheria. Kwa maana nyingine ukiifahamu sheria, utakuwa huru na jamii yako.

Utaweza kulinda na kuitetea jamii yako, ni jukumu la kila mtu au kila Mtanzania kulinda na kuitetea jamii yake dhidi ya vitendo viovu/ukiukwaji wa haki.

Sheria ndiyo inaelekeza hili ni kosa na lile sio kosa, sasa, je, utatambuaje kuwa hili ni kosa kisheria bila kuifahamu sheria au kuwa na dodoso za kisheria? Hivyo jamii itabaki bila utetezi kwani wanajamii hawana haja ya kufahamu misingi ya kuendeshea jamii zao.

Utakuwa na uwezo wa kutetea maslahi ya watu wengine na kulinda maslahi ya taifa lako, maslahi binafsi ya watu na hata maslahi ya taifa kama yamepokwa (chukuliwa) na watu wenye nia mbaya mbele ya macho ya wananchi, na wananchi hawakuchukua hatua zozote kwasababu hawajui kuwa ni wajibu wao.

Wananchi walio wengi hawajui kuwa wana wajibu wa kulinda na kutetea maslahi ya taifa lao.

Ibara ya 27(1)-(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara imeweka wajibu wa kila mwananchi kulinda na kutunza mali za umma, mali zinazomilikiwa na watu kwa ujumla wao pia kuheshimu mali binafsi za mtu mwingine.

Haya yote kila Mtanzania atayafahamu pale tu atakapokuwa na desturi ya kusoma makala mbalimbali za kisheria. Chukua muda wako, soma sheria vizuri (hususan zile zinazoelekeza haki za kiraia na wajibu), ili ufahamu haki na wajibu wako uliowekwa na sheria katika jamii yako.

Ni wazi kuwa sio kila mtu anafahamu au kutambua wajibu wake katika kulinda maslahi na mali za taifa lake.

KUMBUKA: Kutokufahamu sheria hakutakuwa utetezi pale utakapofanya kosa (Kilatini- Ignorancia juris non excusant; Kiingereza-ignorance of the law is not an excuse): Kifungu cha 8, Kanuni ya Adhabu Sura ya 16.

Tena, ili kupunguza matendo maovu kwenye taasisi za umma na binafsi na jamii kwa ujumla ni vema basi tukafahamu sheria. Ile kasumba ya kwamba sheria ni ngumu itoke kwenye kamusi na misamiati ya utashi na akili zetu. Jifunze sheria kwa manufaa yako binafsi na taifa kwa ujumla.



## Kalamu ya Mwalimu

Reubeni Lumbagala

# Wananchi nguzo muhimu ujenzi wa miundombinu ya elimu-1

ILI kutoa elimu bora yenye manufaa kwa wanafunzi na jamii kwa ujumla, suala la miundombinu bora ya kutolea elimu linapaswa kutekelezwa kwa vitendo.

Wanafunzi na walimu wanapaswa kujifunza katika mazingira bora yatakayochochea kujifunza wenye tija. Vyumba vya madarasa, maabara, maktaba, nyumba za walimu, vyoo na ofisi ni miongoni mwa miundombinu muhimu ya kufanikisha kujifunza na una matokeo chanya.

Hivyo, shule zote zinapaswa kuwa na miundombinu bora ya kutolea huduma ya elimu, ili kuifanya iwe bora kwa wanafunzi wanaoipata.

Gharama za kujenga, kuboresha na kukarabati miundombinu ya shule nchini ni kubwa sana, ambayo serikali haiwezi kuifanikisha pekee yake.

Hivyo, mchango wa jamii katika kusaidia kufanikisha shughuli hizo, unapaswa kutolewa ili kuwasaidia wanafunzi kujifunza katika mazingira bora yatakayowavutia kupenda shule na kujifunza.

Serikali inatekeleza kwa vitendo sera ya elimu msingi bila ya malipo. Kila mwezi ni takribani Sh. bilioni 24 zinatolewa kugharamia utekelezaji wa sera hiyo.

Katika kuondoa urasimu wa fedha hizo, serikali inaingiza fedha hizo moja kwa moja katika akaunti za shule, ili zisaidie shughuli mbalimbali kama vile uendeshaji taaluma, utawala, michezo, mitihani, ukarabati au matengenezo madogomadogo, ununuzi wa madawa baridi kwa wanafunzi.

Pia, serikali imetoa fedha nyingi katika ukarabati wa shule kongwe na vyuo vya ualimu kote nchini.

Sambamba na hilo, serikali inatoa fedha katika kufanikisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika shule nyingi za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu.

Hivi karibuni, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alilitaarifu Bunge kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019, serikali imetoa Sh. bilioni 29.9 kukamilisha maboma 2,392 ya madarasa nchini kote.

Naibu Waziri Waitara, alisisitiza kuwa: "Serikali itaendelea kukarabati na kujenga miundombinu ya elimu kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha."

Yote hayo yanafanywa na serikali na yanathibitisha nia njema ya serikali kuhakikisha wanafunzi wote wanasoma katika mazingira mazuri, ili kupata elimu bora. Kwa kuwa serikali imejipambanua kugharamia utekelezaji ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu, wananchi hawana budi kuunga mkono juhudi hizo, ili watoto wao wanaosoma katika shule hizo, wajifunze katika mazingira yanayovutia.

Kuvutia huko kunaelezwa ni kuhakikisha wanachangia rasilimali fedha na nguvu kazi, ili kujenga maboma ya madarasa, ofisi, vyoo, maktaba, maabara na hatimaye serikali kukamilisha maboma hayo.

Msingi wa wananchi kuhamasika kuchangia fedha na nguvukazi katika ujenzi wa miundombinu ya shule wilayani Kongwa, inatokana na elimu inayotolewa na mbunge Job Ndugai, kwa kushirikiana na viongozi wengine wilayani humo.

Hao anawataja ni Mkurugenzi wa Halmashauri na Maofisa Elimu, kwa kuwaambia wananchi kuwa, shule za msingi na sekondari ni mali yao kwa kushirikiana na serikali, hivyo wana wajibu wa kushiriki katika maendeleo yake. Kutokana na hamasa hiyo, wananchi wamejitolea fedha na nguvu kazi katika ujenzi wa maboma ya madarasa, hali iliyosababisha serikali kuunga mkono juhudi hizo za maendeleo kwa kutoa fedha za kumalizia ujenzi ulioanzishwa na wananchi.

Kwa mujibu wa Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Kongwa, Nelson Milanzi, serikali imetoa Sh. milioni 25 kwa Shule ya Sekondari Kibaigwa, kukamilisha ujenzi wa madarasa mawili.

Pia, imetolewa fedha kusaidia shule sita, kila moja ilipatiwa Sh. milioni 25 kukamilisha madarasa yake mawili, ambazo ni katika Sekondari za Makawa, Pandambili, Ng'humbi, Banyibanyi, Mnyakongo, Hembahemba.

Aidha, kuna shule nyingine mbili ambazo kila moja ilipatiwa Sh. milioni 50, kukamilisha madarasa manne kila moja. Hizi ni sekondari za Ngomai na Songambele.

Ofisa Elimu Ufundi Wilaya ya Kongwa Emmanuel Factory, aliongoza kikao cha kujadili ujenzi wa madarasa katika Shule ya Msingi Laikala na wananchi wakakubali kujitolea nguvukazi.

Pia, ahadi yao ni kuwa boma la vyumba viwili na ofisi vinakamilika, ili kuunga mkono ahadi ya Mbunge wa Kongwa Job Ndugai, ya kutoa mifuko 50 ya saruji mara tu wananchi watakapojitolea kuchimba msingi.

Katika hali ya kufurahisha, mafundi wameamua kupunguza gharama za ujenzi, pia kuahidi baadhi ya kazi zitakavyofanyika bure, kwani wao na watoto wao ni zao la Shule ya Msingi Laikala.

**●Reubeni Lumbagala, ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali, iliyoko wilayani Kongwa, Mkoa wa Dodoma. Anapatikana kwa namba: (+255) 764666349.** **Itaendelea Jumamosi ijayo.**

MAKALA

# RTO alipofunga safari kufurahia

## • Mwenye kituo afunguka alivy

Na George Mapunjo




Watoto wanaoishi katika Kituo cha Yatima, Fadhillah, kilichopo Misugusugu, Kibaha, walipotembelewa na wageni.

KATIKA kutetea usalama barabarani ni jambo la ushirikiano, kati ya taasisi zinazotoa elimu ya usalama barabarani na Jeshi la Polisi Tanzania Kitengo cha Usalama Barabarani na wadau wao huchukua hatua za kufanya ushirikiano.

Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani Mkoa wa Pwani na mabalozi wengine, asasi ya Road Safety Ambassodor (RSA), waliungana kula chakula pamoja na watoto yatima wa kituo cha Fadhillah kilichopo Misugusugu, Wilaya ya Kibaha.

Ilikuwa na tafsiri pana, kwamba ilikuwa sehemu ya kuadhimisha siku ya kuzaliwa Kamanda wa Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani (RTO) Mossi Ndozero.

Ni uamuzi aliyoupendekeza kufanya sherehe ndogo ya kuzaliwa kwa kujumuika na watoto hao, kwa lengo la kuwafariji watoto waliopoteza wazazi wao na sasa wako katika vituo vinavyowalea.

Hafla hiyo iliendana na kutoa zawadi aina mbalimbali kama vyakula na mafuta, pia akawapa semina elekezi kuhusu usalama wao wawapo barabarani au kwenye magari pindi wanaposafiri.

Kamanda Mossi, aliambatana na wasaidizi wake aliwaomba wazingatie sheria na kanuni za usalama barabarani na inapotokea tatizo lolote kuhusu usalama wako wakiwa barabarani, hatua gani za kuzifuata kupata haki yako.

Alichokifanya RTO wa Pwani, ni jambo lililofufua tafsiri pana ya wazazi, kwamba haishii kwa watoto aliowazaa au anaowalea, bali hata mtu wa mbali, ambaye anaweza kujumuika naye kufurahi pamoja.

Kujumuika pamoja na watoto yatima na kuwapa semina elekezi ya usalama barabarani, ni jambo jema ambalo wengi wao suala la usalama barabarani bado hawajalifahamu vizuri.

Msingi wa neno yatima, inamwangukia mtoto aliyewapoteza wazazi wake wote wawili na vituo vya kulea watoto vinajitoa kwa hali na mali, kwa ajili ya malezi ya watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu, huku kila siku vikiongeza idadi ya wakazi wake kutokana na uhalisia ulioko katika maisha.

### VITUO VS YATIMA

Imekuwa kawaida hivi sasa takriban kila mkoa au wilaya ina idadi kubwa ya vituo vinavyotoa huduma kwa watoto wasiopata malezi ya kifamilia.

Mbali na serikali, yapo mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyoanzishwa na yanaendelea kuanzishwa kwa minajili ya kuwasaidia watoto wasiopata huduma za msingi kimalezi katika mazingira yao.

Tafsiri rasmi ya kituo cha malezi imeainishwa na Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, kwamba ni nyumba, shule au taasisi inayoendeshwa na mtu au kikundi cha watu, kwa minajili ya kuwatunza watoto wanaohitaji malezi.

Sheria imebainisha sifa za mtoto anayeweza kuishi kwenye vituo hivyo. Kwanza, ni asiyekuwa na familia na asiyeweza kupata malezi sahihi katika familia yake. Kwa idhini ya Ofisa Ustawi wa Jamii, mtoto huyo anaweza kuishi kwenye vituo vya malezi.

Pili, mtoto mwenye wazazi na familia, lakini ambaye kwa maoni ya Ofisa Ustawi wa Jamii, kuishi kwenye kituo cha malezi, ni salama zaidi kuliko nyumbani kwao.

Hapo, inafahamika kuna watoto walio na wazazi wenye matatizo kama ya akili, migogoro mikubwa inayomwathiri mtoto na hata wazazi wenyewe, ambao kwa namna moja au nyingine, wamekosa uwezo wa kumlea ipasavyo.

Tatu, ni mtoto anayelengwa na mgogoro wa kisheria kati ya wazazi wake na shauri linaendelea mahakamani. Mfano, ni mtoto ambaye wazazi wametengana na kila mmoja anahitaji kukaa naye. Katika mazingira hayo, mtoto anaweza kupelekwa kwenye kituo cha malezi, wakati shauri likiendelea mahakamani.

### ALIKOZURU RTO

Msimamizi na mmiliki wa kituo cha Fadhillah, Suraiya Mohamedi, anasema kuna jumla ya watoto yatima 120, wakigawanyika kila jinsi wako 60.

Anasema, kati yao 120 wana matatizo ya kiafya na umri anaowachukua ni kuanzia mtoto mchanga hadi miaka 12, ingawa wanaozidi umri huo anakuwa nao kwa lengo la kuwaendeleza kielimu na baadhi yao hivi sasa wapo ngazi ya vyuo, ikiwamo wanaosomea ualimu.

Suraiya anasema, sababu ya kuanzisha kituo hicho ni huruma aliyoipata, alipomshuhudia aliyeanguka na kuumia sana, ndio ikawa msukumo wa kuanzisha kituo mwaka 2013, ili kuwalea watoto wenye matatizo mbalimbali.

Anajivunia manufaa yake ni kuanzisha na kuwaunganisha watoto wenye matatizo mbalimbali, amefahamiana na watu mbalimbali, pia amekuwa kiungo katika jamii.

Mama Suraiya anasema, awali hakikuwepo kituo cha aina hiyo jirani na anakoishi, akiangukia imani yake kwamba ni 'Ni thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu'.

Anaeleza njia anazotumia ni kupitia familia zenyewe anakohisi kuna shida ya malezi ya watoto, Idara ya Ustawi wa Jamii na Jeshi la Polisi.

### HALI ZAO

Wakati hivi sasa asilimia kubwa ya watoto wananufaika na maisha ya nyumbani, lipo kundi kubwa la watoto yatima zaidi ya 700,000 nchini, wakikosa uhakika wa kupata huduma za msingi.

Takwimu za msingi za elimu nchini mwaka 2016 (Best 2016) ulionyesha Tanzania ina yatima 731,536 waliopoteza mzazi mmoja au wawili, sawa na wastani wa watoto tisa kwa kila 100.

Mikoa yenye viwango vikubwa vya yatima nchini ni Iringa, yenye watoto 14 kwa kila 100 (asilimia 14.4); Njombe watoto 13 (asilimia 12.7); Mbeya kuna watoto 11 na Pwani watoto 10.

Pia, kuna mikoa inayofuatia kwa kiwango kilicho chini ya wastani wa kitaifa wa watoto tisa, vikiwa wastani wa asilimia 8.5 ni mikoa ya Manyara, Kigoma, Singida, Mtwara na Lindi.

Katika kundi hilo la wanafunzi yatima, takribani robo au asilimia 23 wamepoteza wazazi wote wawili, hivyo kutegemea zaidi msaada wa walezi au wasamaria wema.

Mbali na yatima kwa mujibu wa takwimu hizo zilizotolewa kuna wanafunzi wa elimu ya awali 125,141 ambao wamepoteza mzazi mmoja au wote wawili, huku zaidi ya theluthi mbili wakiwa ni wale

MAKALA

# ‘birthday’ na yatima wa Kibaha

## okianzisha, wanavyoishi



wenye mzazi mmoja.

Mwanza inaongoza kwa kuwa na yatima wengi katika elimu ya awali kwa kuwa na watoto 10,848 ikilinganishwa na Katavi yenye wanafunzi yatima 1,168.

Wadau wa malezi na haki za watoto, wanaeleza kuwa yatima ni miongoni mwa makundi ya watoto walio hatarini kutengwa katika jamii na kukosa fursa muhimu katika maisha zikiwamo za kielimu, kijamii na kiafya.

**WASEMALO WADAU**

Asasi ya kiraia ya Save the Children, inatoa ufafanuzi nje ya utafiti kwamba, vyanzo vya baadhi ya mikoa kuwa na yatima wengi ni umaskini, magonjwa kama ukimwi, kifua kikuu na malaria, vifo vya kinamama wakati wa kujifungua na mifarakano katika ndoa.

Japo kuna sababu nyingi za mikoa tajwa kuwa na shida nyingi, moja ya sehemu ni ya matatizo ni kiwango kikubwa cha watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi kwa mujibu wa Takwimu za Utafiti wa Viashiria vya Ukimwi na malaria (THMIS), mwaka 2011/12.

Tofauti na watoto wenye wazazi wote, yatima wanakabiliwa na changamoto nyingi, zikiwamo kukosekana walezi imara na wenye mapenzi kwao, jambo linalowafanya watoto wakose haki na fursa nyingi za kujiendeleza kimaisha.

“Tafiti zinaonyesha kuwa yatima huwa na changamoto za kifedha na vikwazo vingine vya kupata elimu, hivyo huwa katika hatihati ya kukosa elimu bora, ambayo ingewapa fursa ya kujikita kwenye taaluma zinazohitaji ujuzi wa juu na kupata ajira zinazolipa zaidi,” kwa mujibu wa utafiti wa Save the Children.

Mbali na kukosa elimu, yatima wapo hatarini kupata msongo wa mawazo na matatizo ya kisaikolojia, chanzo ni kukosa malezi kamilifu, hasa kutoka kwa wasio walezi wa uhakika, hali inayowazuia kufurahia utoto wao na kuishi kwa afya.

**CHANGAMOTO**

Yatima wanakumbana na changamoto za ulinzi katika familia na jamii, jambo linalowasogeza kuwa waathirika wakubwa wa mimba na ndoa za utoto, zinazowaengua kutoka kwenye fursa za kimasomo.

Hata hivyo, watoto hao wanaweza kulelewa katika mazingira mazuri ambayo yatawafanya wapate fursa nyingi kama wenye wazazi wote wawili.

Kuhusu kitua cha Fadhillah, Suraiya anataja changamoto zake ni usumbufu anaopata kupitia hao vijana kama vile tabia ya utundu.

Anakiri jamii kumpatia misaada mingi ya kuwahudumia watoto hao, ingawa bado anaomba wafadhili wazidi kujitokeza kumsaidie kutimiza lengo aliloanzisha kuwasaidia yatima hao.

Inaelezwa kitaalamu, mafanikio dhidi ya madhila kwa yatima, yanaweza kupatikana kupitia utekelezaji wa sheria, sera na miongozo inayohusu maslahi na ustawi wa watoto kama vile Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.

Ni mambo yanayoendana na maboresho ya sheria hasa zote zinazomkandamiza mtoto, ikidokezwa na wataalamu kuhusu maeneo kama Sheria ya Ndoa nchini, bado inachangia kuwapo yatima, hasa kwa jinsia ya kike kupitia ndoa na mimba za utotoni.

Hapo ndipo inapoingia haja ya nafasi ya serikali katika ngazi mbalimbali kuchukua hatua ya kuwatambua na kuwalinda yatima, inayosaidia kupatikana takwimu za wanafunzi yatima shuleni.

Lingine linaloingia katika mtazamo huo, ni hoja ya kuanzishwa mfuko wa elimu wa kila mkoa, unaolenga kuwawezesha wanafunzi wote wanaosoma katika mazingira magumu hususan yatima.

Pia, katika upande wa pili inabeba umuhimu wa uwezeshaji watoto wanaoishi mazingira magumu, kupitia chombo kama mpango wa kitaifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.


Malezi ya yatima ni mtambuka na yanahusisha taasisi na watu mbalimbali. Jambo linalosisitizwa ni kutimiza haki zao za msingi, ekimu ikiwa mojawapo.

**Mwandishi ni mwalimu kitaaluma anapatikana kwa simu. (+255) 0717 314 100**



Kamanda wa Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani, mkoa wa Pwani, Mossi Ndozero, akigawa zawadi kwa yatima katika kituo cha Fadhillah kilichopo Misugusugu, wilayani Kibaha. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 5 00)



**Dondoo: Kulia**

1. Mtu mjinga
8. uwezo wa juu wa kuongoza 9. maarifa
11.Mji mkuu wa Norway
13.mamlaka ya utawala fulani
14.Rhodesia ya kusini sasa
16.Silaha yenye kudhuru
18.sehemu ya kitu
20.Fanya jambo pasi lazima
21.Mjumbe wa Mungu
23.Eneo la Kush zamani
24.Mnyanganyi aviziaye watu
25.Tayarisha

**Dondoo: Chini**

1. Mto wa 4 kwa urefu Afrika
2. Mzazi wa kike
3. Tendo la kusambaza taarifa
4. Ukoo
5. Chakula cha taifa
6. Ugwe
7. Mahali penye mwinuko
10.zuia jambo lisifanyike
12.tamasha
15.Mwanamuziki
17.Patiwa msaada
19.Kinyume cha wembamba
22.Mdudu aletaye malaria
23.Dhamira

**Jibu na: 4**

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| E | V | E | R | E | S | T | | A | M | A | N | A |
| D | | K | | L | | O | | L | | N | | |
| W | A | S | H | I | N | G | T | O | N | D | C | |
| A | | I | | M | A | O | R | I | | A | | K |
| R | | R | A | I | S | | E | | A | M | U | A |
| D | | E | | S | A | I | N | I | | A | | N |
| L | | I | | H | | | I | | | N | O | A |
| O | | | K | A | A | | | U | F | A | | D |
| W | E | Z | I | | T | O | B | O | | | | A |
| A | | | U | | H | | A | T | I | B | U | |
| S | H | A | M | B | A | | B | O | G | O | T | A |
| S | | | B | | R | | U | | A | M | U | |
| A | | S | E | M | I | N | A | | | A | | |



Waandishi wa habari kutoka mataifa ya Tanzania, Zambia, Zimbabwe, Guinnea Bissau, Rwanda, Kenya, Ghana na Liberia wakiwa katika mkutano mjini Kigali, Rwanda wakijadili matatizo yanayowakabili watoto wa kike na wanawake Afrika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waandishi waazimia kuimarisha vita unyanyasaji wa wanawake

**Na Gwamaka Alipipi, aliyekuwa Kigali, Rwanda**

## ▪Ni katika mkutano wao jijini Kigali nchini Rwanda

VITENDO vya unyanyasaji, ukandamizaji na ukatili kwa wanawake bado vinaendelea katika jamii mbalimbali barani Afrika.

Matukio kama vile kukeketwa, kuchomwa sehemu za siri, kubakwa, kunyang'anywa mali, kurithiwa, haki ya uzazi wa mpango ni baadhi ya matukio yanayozidi kushamiri siku hadi siku miongoni mwa jamii.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linalojihusisha na idadi ya watu (UNFPA), kati ya wanawake na watoto wa kike milioni 100 hadi 140 wanafanyiwa vitendo vya ukeketaji.

Vilevile, kati ya wanawake na watoto wa kike milioni tatu hadi nne kutoka nchi za Kenya, Uganda, Tanzania, Somalia na Ethiopia wanakeketwa kwa mwaka.

Aidha, zaidi ya wanawake 800 hufariki kila siku kutokana na matatizo ya utoaji mimba.

Takwimu zinabainisha kwamba takribani wanawake na wasichana milioni moja wanafariki kutokana na vitendo vya kikatili, vingi vikiwa ni matunda ya tamaduni zilizopitwa na wakati.

Madhira haya ndiyo yaliwagusa waandishi wa habari 35 kutoka mataifa nane barani Afrika kukusanyika pamoja jijini Kigali nchini Rwanda na kuzungumza kwa pamoja kuhusu kadhia hiyo, kisha kuja na kauli moja iliyoazimia kuvitokomeza vitendo hivyo.

Azimio lililotolewa ni la kuzitaka serikali za nchi za Afrika kusimama imara kumsaidia mtoto wa kike na mwanamke dhidi ya mila potofu, pamoja na kuzifanyia marekebisho sera na sheria zilizopitwa na wakati ambazo zinamkandamiza na kumgusa moja kwa moja mwanamke.

Waandishi kutoka nchi za Ghana, Rwanda, Tanzania, Liberia, Zambia, Zimbabwe, Kenya, pamoja na Guinea Bissau walikutana kwa siku nne kumjadili mwanamke na namna ya kumkomboa.

Shirika la Haki za Wanawake barani Afrika (Femnet) ndilo lililoratibu mkutano huo likiwa na lengo moja tu ambalo ni kumweka mwanamke huru kutoka katika vitendo vinavyomnyima uhuru, kumkandamiza na vile vinavyomnyima uhuru wa kutimiza ndoto zake katika maisha.

Wakizungumza kwenye mkutano huo, waandishi hao walieleza namna baadhi ya sheria zilizopo nchini mwao, zinavyochangia moja kwa moja kumkandamiza mwanamke.

Sally Chiwama, mwandishi mwandamizi aliyebobea katika kuhabarisha habari za haki za wanawake nchini Zambia anasema nchini kwake, serikali bado haijajitoa kwa asilimia 100 kupambana na mila na tamaduni potofu dhidi ya mwanamke.

Anasema vitendo kama ukeketaji, ndoa za utotoni, mjane kurithiwa bado vinaendelea katika baadhi ya jamii, huku serikali ikifumbia macho.

"Ni aibu kubwa japokuwa tuna sera na sheria barani Afrika, lakini bado matatizo yanaendelea... japokuwa waandishi wa habari tunaripoti na kuandika matukio haya, lakini bado serikali zetu hazitaki kufanya mapitio upya ya sheria hizo," anasema Chiwama.

Kwa upande wake Gloria Tamba ambaye ni mwandishi kutoka Liberia anasema nchini kwake ongezeko la vifo vya wanawake na watoto wa kike kutokana na vitendo vya ukatili linaendelea, lakini serikali inaangalia tu bila kuchukua hatua madhubuti.

Anasema licha ya waandishi wa habari kuandika mara kadhaa habari zinazohusu vifo vya wanawake na watoto wa kike, lakini bado serikali haijachukua hatua yoyote ya kuhakikisha suala hilo linadhibitiwa.

"Watoto wa kike na wanawake bado wanakufa kwa matukio yanayoweza kudhibitiwa, lakini serikali ipo na inaangalia tu bila kuchukua tahadhari yoyote ya kupambana navyo...sisi kama waandishi wa habari tusichoke kuandika na kuripoti matukio hayo," anasema Tamba.

### MKURUGENZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Femnet, Memory Kachambwa, akitoa neno kwa waandishi hao wa habari anavitaka vyombo vya habari barani Afrika kuhakikisha vinahimiza serikali zao kupambana ili kuhakikisha idadi ya vifo vya wanawake na watoto vinatokomezwa.

"Ninajua kwenye kila nchi barani Afrika kuna sera na sheria zinazomlinda mwanamke na mtoto wa kike, lakini utekelezaji wake ni sifuri, na hii ndiyo maana serikali za Afrika zinatakiwa kuchukua hatua zaidi... haitoshi kuwa na maazimio kwenye karatasi peke yake bali utekelezaji ni muhimu," anasema.

Anasema kati ya nchi 20 duniani zenye idadi kubwa ya vitendo vya ndoa za utotoni, 15 zipo Afrika.

Anabainisha kwamba inakadiriwa kila siku watoto wa kike 37,000 chini ya miaka 18 wanalazimishwa kuolewa, jambo ambalo linasababisha kukatishwa masomo yao na hivyo ongezeko la umaskini.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyu, inakadiriwa ifikapo mwaka 2050, matukio ya ndoa za utotoni barani Afrika yatafikia milioni 310 kulingana na ukuaji wa idadi ya watu.

Aidha, anasema vitendo vya vitisho kwa watoto wa kike na wanawake bado vinaongezeka katika nchi nyingi barani Afrika, Kenya ikiwa ni mojawapo ya mfano.

"Kesi za ubakaji wa watoto wa kike na wanawake nchini Kenya zinakadiriwa kufikia 40,000 kwa mwaka, na zinazoripotiwa ni 4,000 tu," anasema.

Merceline Nyambala ni mwandishi wa habari kutoka Kenya ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Kenya (AMWIK).

Nyambala anabainisha kwamba kunahitajika umoja wa hali ya juu miongoni mwa waandishi wanawake Afrika kuhakikisha wanawake na watoto wa kike wanapewa nafasi katika kueleza matatizo wanayokumbana nayo.

"Tumeshaona madhara yanayotokea kwa watoto wa kike na wanawake katika nchi zetu, sasa ni wakati wetu wa kuhakikisha serikali inakuwa sehemu ya mapambano ya kumkomboa mtoto wa kike," anasema.

Anafafanua kuwa waandishi wa habari wanapaswa kuripoti na kuandika mara kwa mara habari zinazohusu jinsia, kwani zitasaidia kuleta mabadiliko katika jamii.

Kadhalika, anavitaka vyombo vya habari hususani redio na televisheni kuzipa muda mwingi mada za jinsia, huku vyombo vya magazeti zikiandika makala nyingi zinazohusu wanawake.

"Wanawake wengi wanafariki kwa sababu ya unyanyasaji wa kijinsia, wakati wa kujifungua, pamoja na tamaduni zilizopitwa na wakati... ni jukumu letu kukemea kupitia kalamu zetu, kila serikali barani Afrika inapaswa kusimama na kukemea," anasema Nyambala.

Anabainisha kuwa ni kipindi kirefu sasa utu wa mwanamke na mtoto wa kike umekuwa hauthaminiwi, na kwamba sasa hali imekuwa mbaya zaidi kuliko kipindi cha wakoloni.

HABARI KIMATAIFA

# Wabunge wasusia bajeti kisa mwenzao kupigwa

**NAIROBI, Kenya**

WABUNGE wanawake nchini Kenya wamesusia kikao cha bajeti wakilalamika hatua ya mwenzao kudaiwa kushambuliwa katika majengo ya bunge na mbunge wa kiume.

Wabunge hao walitaka Mbunge wa Jimbo la Wajir Mashariki, Rashid Amin, kukamatwa kwa kumpiga mbunge mwakilishi wa wanawake wa jimbo hilo, Fatuma Gedi.

Tukio hilo lilitokea wakati Bunge liliporejelea kikao cha mchana cha usomaji wa bajeti.

Wabunge hao walisikika wakiimba nyimbo za kumtaka Mbunge Rashid na Mbunge Aden Duale wajiuzulu.

Wanawake hao walimlaumu Duale kwa kushindwa kuwatetea viongozi wanawake bungeni.

Spika wa Bunge la Kenya, Justin Muturi, alilazimika kuwaita maofisa wa ulinzi wa Bunge na kuwatoa nje wabunge waliokuwa wakizua vurugu muda mfupi kabla ya kusomwa kwa makadirio ya Bajeti ya mwaka 2019/2020.

"Walinzi wa bunge watoeni wabunge wote wanaopiga mayowe katika ukumbi wa Bunge," alisikika akisema Muturi.

Licha ya agizo la Muturi, lakini viongozi hao waliokuwa na hasira waliendelea kupiga mayowe wakisema: "Hatutanyanyaswa na wanaume, tumechoka hadi pale agizo la Spika lilipotekelezwa."

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa Rashid alimshambulia Fatuma katika eneo la kuegesha magari baada ya wao kutofautiana vikali kabla ya kumzaba makofi mbele ya walinzi wao.

Vyombo vya habari nchini Kenya vinaripoti kuwa Rashid alitaka kujua kwa nini Gedi ambaye ni mwanachama wa kamati ya bajeti, hakuitengea mgao wa fedha Jimbo la Wajir Mashariki, wakati kamati ya bajeti ilipozuru eneo hilo hivi karibuni.

Mwakilishi wa wanawake wa Jimbo la Homabay Magharibi mwa Kenya, Gladys Wanga alisema alishuhudia tukio hilo kwani alikuwa akiandamana na Gedi.

Katika picha iliyosambazwa, Gedi anaonekana akitokwa na machozi, kadhalika akionekana kuwa na matone ya damu mdomoni.

Kisa hicho kimezua mjadala mkali katika mitandao ya kijamii nchini Kenya, huku wengi wakimlalamikia Rashid kwa kitendo alichokifanya.

Kwa kutumia hushtag #JusticeForFatumaGedi katika mtandao wa kijamii wa Twitter Wakenya wamekuwa wakishinikiza mbunge Rashid achukuliwe hatua kali.

Tayari Mbuge Fatuma Gedi amewasilisha rasmi ripoti kwa polisi kuhusiana na kisa hicho, Rashid anazuiliwa katika kituo cha polisi.

Hata hivyo, purukushani iliyotokea bungeni ilichukua karibu nusu saa kutulia, na Bunge likaendelea.

*BBC*




Maofisa afya nchini Uganda wakichukua tahadhari kwa kuwapima wananchi wanaowahisi wameambukizwa ugonjwa wa ebola. **PICHA: ALLIANCE**

# WHO wakutana kujadili ebola

**KAMPALA, Uganda**

JAPO la wataalamu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) limekutana kwa dharura Ijumaa, ili kuamua iwapo litangaze ugonjwa wa ebola kuwa ni kitisho cha kimataifa baada ya ugonjwa huo kusambaa nchini Uganda.

Kamati ya dharura ya shirika hilo iliyoanzishwa mwaka 2005, imewahi kutangaza milipuko minne ya magonjwa kuwa kitisho cha kimataifa, ikiwamo ugonjwa wa homa ya nguruwe, mlipuko wa ebola katika nchi za Afrika Magharibi kati ya mwaka 2014 hadi 2016 pamoja na virusi vya zika.

Mgogoro wa sasa wa ebola, ambao ulianzia Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (Congo) umeshuhudia matukio 2,000 yakitokea ya wagonjwa wa ebola na theluthi mbili kati yake yalikuwa mabaya sana. Jopo hilo la WHO, linalojulikana kama Kamati ya Dharura ya Kimataifa ya Kanuni za Afya, limekutana mara mbili kuhusiana na mlipuko wa ugonjwa huo nchini Congo.

Katika mikutano yake hiyo miwili, haikuutangaza ugonjwa huo kuwa kitisho cha ulimwengu kwa sababu haukuripotiwa katika nchi nyingine.

Lakini hali ilibadilika ghafla wiki hii baada ya watu wawili kuthibitishwa kufariki kwa ugojwa huo Magharibi mwa Uganda.

Mwanamke mmoja raia wa Congo aliyeolewa na Mganda, pamoja na mama yake na watoto watatu na mlezi wao walisafiri hadi Congo kwa ajili ya kumuuguza baba yao aliyekuwa na maambukizi ya ebola na baadaye kufariki. Shirika la Afya limesema wanafamilia 12 ambao walihudhuria mazishi nchini Congo waliwekwa katika sehemu maalum, lakini sita kati yao walitoroka na kurudi Uganda Juni 9.

Kwa mujibu wa WHO, mwanaume huyo anayedhaniwa kuwa ndiye aliyesababisha kusambaa kwa ebola nchini Uganda alikuwa ni mchungaji na alikuwa hajulikani na maofisa wa afya kabla ya kufariki.

Mkuu wa Kamati ya Dharura ya WHO, Dk. Mike Ryan, alisema mchungaji huyo hakuwa kwenye orodha ya watu walio katika hatari ya kupata virusi vya ebola.

Kamati hiyo ya dharura inasema hakuna ushahidi kuwa ebola imesambaa Uganda, kwa sababu hadi sasa mlipuko huo umeripotiwa katika mkoa mmoja na kwamba mamlaka zinawafuatilia kwa karibu wanafamilia wote ambao wanashukiwa kuwa na maambukizi yake.

Wakati huo huo, utafiti mpya kutoka Chuo Kikuu cha Cambridge unaashiria kuwa nusu ya milipuko ya ebola haikuweza kugundulika tangu virusi hivyo vilipojitokeza kwa mara ya kwanza 1976.

*DW*

## Rais Salva Kiir amtumbua Waziri wa Mafuta

**JUBA, Sudan Kusini**

RAIS wa Sudan Kusini, Salva Kiir, amemfuta kazi Mkuu wa Wizara ya Mafuta, Ezekiel Lol Gatkuoth na kumteua Awow Daniel Chuang kuongoza wizara hiyo.

Wizara ya Mafuta Sudan Kusini inaingiza asilimia 90 ya mapato yote ya serikali. Gatkuoth ameongoza wizara hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu

Hata hivyo, Rais Kiir hakutoa sababu za kufanya mabadiliko hayo lakini mchambuzi wa masuala ya kiuchumi mjini Juba alieleza labda Gatkuoth alifukuzwa kazi kwa sababu hakuwa muwazi namna fedha za wizara hiyo zilivyokuwa zikitumika na pengine alivunja sheria kwa kuweka fedha ndani ya akaunti kwenye benki ya serikali.

Naye mchambuzi wa sera, Augustino Ting Mayai wa Taasisi ya SUDD yenye makao yake Juba alieleza kwamba katika mwaka wa kwanza wa Gatkouth kama Waziri wa Mafuta, uzalishaji mafuta na mapato kwa serikali ulipungua wakati mzozo ulipokuwa unaendelea nchi humo, hata pale bei ya mafuta iliposhuka kwenye soko la kimataifa.

**VOA**

## DRC yaomba kuwa mwanachama wa EAC

**KINSHASA, Congo**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi, amesema nchi yake hivi karibuni imeomba kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

DRC inapakana na mataifa nane kati ya sita ambayo ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambapo Rais Tshisekedi alisema moja ya dhumuni ya ziara yake nchini Tanzania ni kusisitiza ombi lao ili kurahisisha masuala ya kibiashara.

Rais Tshisekedi alisema kuingia na kuwa mwanachama wa jumuiya hiyo kutasaidia kupunguza vikwazo vya kibiashara na kuongeza tija katika ufanyaji biashara baina ya mataifa yao.

Akiwa nchini Tanzania Rais Tshisekedi alitembelea Bandari ya Dar es Salaam ambayo kwa sehemu kubwa inatumiwa na nchi yake kupitisha mizigo.

**RFI**

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# Jumba Jekundu-5

**Na Adam Fungamwango,**

**(0716 350534)**

Aliamua kujitosa kwenye mvua kwenda kwenye duka la Meze kununua unga, nusu kilo kwa ajili ya chakula cha mchana yeye na familia yake.

Alikuwa anakwenda hatua kwa hatua, nyumba kwa nyumba, kwa sababu ya mvua. Anatoka nyumba hii na kukimbilia nyumba nyingine anasimama.

Alifika dukani. Ndani ya duka kulikuwa na Meze pamoja na Kadili. Kutokana na tabia yake ya umbea, mama Gombea alisikia sauti na kutaka kujua nini kinaongelewa kabla ya kujitokeza dukani na kununua alichokihitaji.

Ndipo aliposikia mazungumzo ya vijana hao kuhusu msichana waliyekuwa naye kwenye hoteli ya 'Blue Star'. Na ndipo taarifa hiyo alipoipeleka kwa mama Kadili.

Hata hivyo ilikuwa ni taarifa ambayo haikukamilika kwa sababu hakuelewa vitu vingi kwa sababu hata Kadili na mwenzake Meze bado walikuwa hawajajua vitu vingi kuhusu yule msichana.

Alichosikia ni vitu vichache tu.

"Mwanangu mimi nakwambia ukweli, yule msichana amekuzimikia."

"Wee Meze acha wee, siyo kweli sema yule mtoto kazimika jinsi nilivyokuwa nacheza tu."

"Hakuna yule mtoto wa kitajiri kakupenda, mimi nawajua mademu wa aina ile."

"Kusema kweli jinsi alivyo mwanangu, hata mimi nimempenda, ila yale maji marefu kwangu."

"Maji marefu gani Kadili wakati mtoto wa kishua kakupenda mwenyewe?"

*******************************************

"Ebwana eee, hii inshu yetu mbona naona kama mama kashtukia hivi?" Kadili alimuuliza mwenzake.

"Inshu gani, hii ya yule demu?"

"Ndiyo, maana siku ya tano sasa mama kang'ang'ania kuwa nimebadilika, mara mimi nakujua ukiwa na raha na ukiwa na huzuni."

"Wewe Kadili nawe umezidi, tangu ukumbatiwe na yule mtoto wa kishua umebadilika, umekuwa kama mtu wa mawazo hivi. Sasa kinachokufanya uwaze nini? Huamini kama yule binadamu, umekumbatiwa na jini, au vipi?" Meze aliuliza kimzaha.

"Mimi mwenyewe hata sijielewi. Unajua mimi sijui kama nimebadika, najiona niko vile vile, lakini mama yeye ndiyo ananiambia nimebadilika."

"Hata mimi nakuona siyo Kadili yule. Mtoto kakuletea tabu yule."




"Sasa unasikia, jana sasa, nasikia mama anasema, tusubiri kuletewa mkwe hapa siku si nyingi. Sasa mimi nikaona kabisa hii nitakuwa naambiwa mimi, wala si dada zangu, nikaona kama taarifa zinavuja hivi."

"Unataka kunituhumu kwamba mimi ndiye ninayevujisha siri?"

"Siyo hivyo Meze, nina wasiwasi kuwa tunavyoongea mambo yetu, huenda kuna mtu anatusikia, au kuna siku mtu katusikia, halafu anajua na mama kaenda kumwambia."

"Mhh! Sijui, inawezekana lakini."

Yalikuwa ni mazungumzo ya Kadili na Meze kama kawaida yao wakiwa dukani.

Hawajui kuwa mama Gombea ndiye aliyemmegea taarifa mama Kadili, baada ya kuzisikia wakiwa hapo hapo dukani.

"Sasa unaonaje Jumamosi twende tena?" Kadili alianzisha tena mazungumzo baada ya kimya kwa dakika moja kumpisha mwenyeji wake kumhudumia mteja.

"Nilijua tu, isingekuwa rahisi wewe kukaa ukimuwaza yule dada bila kwenda tena 'Blue Star'."

"Si rahisi Meze, mimi nataka kujua hatima ya yote yale."

"Lakini atakuja? Isije kuwa alikuja siku ile tu."

"Tutajua hapo hapo."

"Na kama akija, atakufuata tena kucheza na wewe, au ilikuwa siku ile tu ilikuwa ngekewa?"

Swali hili lilimuingia vilivyo Kadili. Naye alikuwa akijiuliza hivyo. Ni kweli mrembo yule kama watamkuta anaweza hata kuongea naye, achilia mbali kucheza naye kama wiki mbili zilizopita?

Atamchangamkia kama siku ile? Wanaweza kucheza naye muziki kama siku ile? Na kama vyote vikiwezekana kuna chochote kile ambacho anaweza kumwambia? Jibu lilibaki pale pale kuwa ni hapana.

Kadili hakuwa na chochote ambacho cha kumvutia mrembo yule kiasi cha kuvutika kuwa naye.

Hata hivyo, alichojali zaidi ni faraja. Faraja ya kusalimia na kuthaminiwa na msichana mwenye hadhi na urembo wa aina ile.

Ila jambo moja tu lilimuumiza. Kama akimchunia tu na kumchukulia kama siku ile ilikuwa ni zari yake tu ya kucheza naye itakuwaje?

"Nitaumia moyoni." Alijisemea.

**********************************

Ilikuwa ni Jumamosi nyingine ndani ya hoteli ya Blue Star Sinza. Kama kawaida ya hoteli za kisasa, mara nyingi hujaa wateja wengi kutokuwa na upya wake.

Wengi wanataka kuweka rekodi kuwa hoteli ile alishawahi kuingia na kunywa.

Mapema tu, Kadili na rafiki yake Meze walikuwa wameshatinga na kukaa kwenye ukumbi wa watu wanaokunywa.

Siku hii waliingia tofauti kidogo. Waliingia na hofu. Siku ya kwanza waliingia kwa kujiamini na lengo lao kwenda kufurahi na kucheza muziki, ikiwamo kushindana.

Zamani walipokuwa watoto walikuwa hawashikiki na hawashindikani kwa kucheza muziki kwenye sherehe mbalimbali mtaani kwao kiasi cha kuzawadiwa pesa na kuzungukwa na kupigiwa makofi na kushangiliwa na watu mbalimbali.

Siku ya kwanza walionekana kuwa hawajapoteza sana ule uwezo wao, badala yake walionekana kidogo wazito kutokana na kutokuwa na tabia ya mara kwa mara ya kwenda disco.

Kwa bahati alitokea mwanadada huyo aliyevutiwa na uchezaji maridhawa wa Kadili na kumfuata kucheza naye.

Safari hii hawakuonekana kuwa na amani moyoni. Walichofuata si kucheza disco kwa asilimia 100 kama siku ile. Ila kumuona yule mrembo.

Kwa muda wa saa moja na nusu waliokaa hapo hakukuwa na dalili yoyote ya kuwapo kwa aina ile ya msichana. Kila mmoja alikunywa bia tatu, ingawa walitumia muda mrefu kidogo.

Waliamua kuinuka kwenye ukumbi wa vinywaji na kuingia kwenye ukumbi wa kucheza muziki.

Walisimama tu. Hakuna hata mmoja aliyekuwa na hamu na kucheza muziki. Kila mmoja alimuwaza mrembo wa siku ile.

Ghafla kuna mtu mmoja aliingia kwenye ukumbi wa kucheza muziki. Hakuna mgeni machoni mwa Kadili na mwenzake. Walimuona wapi?

Wakati anarudisha kumbukumbu nyuma na kuweza kukumbuka kuwa alikuwa ni mmoja wa mabaunsa aliowaona wiki mbili zilizopita wakimchukua msichana yule, nyuma yake aliingia mrembo ambaye amemfanya kutokuwa kwenye hali ya kawaida kwa muda wa wiki mbili sasa.

Macho ya Kadili na Meze yakagongana. Wakaangaliana. Walishindwa kuongea kitu chochote. Miguu ilianza kucheza Kadili. Mdomo pia ni kama ulikuwa umefungwa na kufuli gumu. Hakuweza kuinua hata hatua moja ya mguu.

Waliyemuona siku ile alikuwa amependeza mara kumi zaidi kuliko siku ile. Alionekana ni malkia haswa.

Kuna dhana imejengeka kuwa baada ya miaka 50, malaika mmoja hudondoka duniani. Huenda mmoja wao ni huyu. Kadili aliwaza.

Urembo, mavazi yake ya gharama yaliupamba usiku ule pamoja na ukumbi ule. Harufu mpya nzuri ya pafyumu, ilibadilisha hewa ya ukumbi ule. Kadili alijihisi kama anashindwa kuhema.

Mabausa watatu wale wale wa siku ile ya kwanza, walikaa pembeni kabisa mwa ukumbi na kumuacha binti yule akicheza disco peke yake taratibu.

Kadili alitaka kusogea katikati ya ukumbi ili acheze na kuonekana na mrembo yule, lakini miguu yake ilionekana kuendelea kutompa ushirikiano kwa kutetemeka. Alibadi amejikunyata kama mtu anayeona baridi.

Bahati ni kwamba wengi waliokuwa wakicheza hapo walikuwa na wenzi wao, ndiyo maana ilimpa fursa mrembo huyo kucheza peke yake, ingawa mibaba hiyo hiyo iliyokuwa ikicheza na wapenzi wao, ilikuwa ikiiba jicho na kumtazama mrembo huyo, wakiushangaa uzuri wake, mioyo yao ikiburudika.

Kwa mbali jicho la mrembo huyo ni kama lilimuona Kadili. Mwenyewe alibaki amesimama akiwaangalia wanaocheza, huku akijua mrembo yule ama amemsahau, au kwa siku hiyo hakuwa na mpango wowote na yeye.

Mrembo alioneka kucheza akisogea eneo lile. "Vipi swahiba, leo unaumwa." Ni sauti ambayo ilipenya si kwenye sikio la Kadili tu, lakini mpaka moyoni.

Ilikuwa ni sauti ya msichana yule ambaye alionekana kumkumbuka Kadili, lakini pia kumfuata na kwenda kumsalimia.

Kwa vyovyote ambavyo ingekuwa, Kadili asingeweza kumfuata msichana yule na kwenda kumsalimia.

"Hapana, siumwi, ila naangalia tu watu wanaocheza."

"Siku ile ulicheza vizuri sana, leo njoo tucheze tena wote, leo na mimi nitakuonyesha kuwa najua zaidi kuliko wewe." Aliongea kwa sauti ya mzaha, iliyokuwa nyororo na tulivu.

Maneno yote yale na yaliyotokea kwa Kadili kwake ilionekana kama ni ndoto. Alibaki amesimama, kabla ya mrembo hule kumshika mkono na kumvuta katikati na kucheza naye muziki.

Meze naye alijitosa kucheza muziki, huku akimuangalia kwa chati rafiki yake aliyekuwa chini ya himaya ya mrembo ambaye hawamfahamu, lakini ni kama ameondokea kuuteka moyo wake, lakini kikwazo kikubwa kikiwa ni hadhi.

Baada ya ngoma nne, hivi, kila mmoja kucheza kwa bidii, mrembo alisogeza mdomo wake kwenye sikio la Kadili.

"Unaitwa nani?"

"Kadili."

"Ok, unaishi wapi?"

"Naishi Tandale Kwa Tumbo."

"Nashukuru kukufahamu swahiba, mimi naitwa Edina, naishi Oysterbay."

***ITAENDELEA JUMAMOSI***

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MAGARI NA VIPURI**

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,
2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz ,au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI



**Hajara H. Muro** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0531-0019** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013, katika shule ya Sekondari Ruaha. Yeyote atayekiona atoe taarifa. Polisi Taarifa: **IRI/IRI/RB/57177/2019**

115275602


## KUPOTEA KWA CHETI



**Mengi A. Kamba** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0432-017** kilicholotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1989, katika shule ya Sekondari Jabal-Hira Muslim Juniour Seminary. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **PWA/KIB/RB/61956/2019**

115275802

## CHETI KIMEPOTEA



**RAYMOND MBWANA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0465/0245** kilichotolewa na JAMHURI SEKONDARI mwaka 1999.Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/57863/2019.**

115276402

## CHETI KIMEPOTEA



**ANSELMINA MAHUWI** anatangaza kupotelewa na cheti cha **KIDATO CHA NNE** chenye no P0377-0008 kilichotolewa na NECTA TANZANIA mwaka 1998 Shule ya Lugalo High school. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/60024/2019**

215275501

## KUPOTEA KWA KADI

**Tanzania Beijing Huayuan Security Guard Services** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili **MC 421BER** aina ya KINGLION. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KW/BI/1/VILXI/141**

115277002

**IN THE COURT OF DISTRICT DELIGATE OF DODOMA**

**AT DODOMA**

**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO.37 OF 2019**

**In the matter of the Estate of the late VICENT ELISHA MSAMBAZI-PETITIONER**

**And**

**In the matter of Application for letters of Administration by EGLA WILLIAM KUTIMWA**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before 3RD /07/2019.

Dated at Dodoma this ….14TH /06/2019

Resident Magistrate
DODOMA.

115276602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;126/2019**

**Ombi la JOHSON LAURIAN KAZIMILI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu KAZIMILI PASCHAL SHOMARI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 28/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 12/06/2019.

115276902

## KUPOTEA KWA KADI

**Herman Samweli Shao** anatangaza kupotea kwa kadi yenye usajili wa namba **T513 BRP** aina ya **M/FUSO.** Yenye chasis namba **FK618D521347.** Yeyote atakaeziona ataoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/KIJ/RB/61914/2019**

115276802

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**TULIBAKE JUNTWA MWALYAJE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 559 DPV TOYOTA IST.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **SO/RB/4446/2019.**

115276502

## KUPOTEA KWA KADI

**Amina Ramadhani Mbisha** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T721 DDJ** gari aina ya **TOYOTA PORTE,** yenye chasis namba **NNP110046392.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi taarifa: **DAR/KJN/61506/2019**

115276702

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
15/06/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 15/06/2019 Kampuni ya **Musa holding** itapitisha gari lenye vipimo vya tofauti kutoka Moshi -Mwanga gari lenye namba za usajili **T277ALQ.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   - **Urefu - 9.7**
   - **Upana - 3.0**
   - **Kimo - 3.0**
3. Njia itakayotumika ni **Moshi - Mwanga**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115276002

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
16/06/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumapili tarehe **16/06/2019** Kampuni ya **Musa holding** itapitisha gari lenye vipimo vya tofauti kutoka **Mwanga - Moshi** gari lenye namba za usajili **T277ALQ.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   - **Urefu - 9.7**
   - **Upana - 3.0**
   - **Kimo - 3.0**
3. Njia itakayotumika ni **Mwanga - Moshi**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215276002

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
14/06/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe **17/06/2019** kampuni ya **Builders & Limeworks Co. Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **ARUSHA kuelekea MOSHI,** gari hilo lenye namba za usajili **T170 BAP/ T515 ALG**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   - **Urefu ……………….. 17.0m**
   - **Upana ………………… 3.5m**
   - **Kimo ………………… 4.55m**
3. Njia itakayotumika: **ARUSHA hadi MOSHI Kupitia KIA,** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215275902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI/TRAILER

**Z.H. POPPE LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya IVECO yenye namba za usajili **T 342 AVG.** Kadi ya gari aina ya TRAILER yenye namba za usajili **T 101 DAV.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Control **No. 991088146015.**

115276302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
***(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)***

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 45/2019**

**Ombi la - JACOB MWAKIBIBI**
**- ELIZABETH KIMARO kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu BUPE SHYLOCK KIMARO.**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 1/07//2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 13/6/2019

215276102


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SALAH AJIUNGA KIKOSI CHA MISRI

**LIVERPOOL, England**

WINGA wa Liverpool, Mohamed Salah, amejiunga na kambi ya timu ya taifa ya Misri kwa ajili ya maandalizi ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), zitakazofanyika Misri mwezi huu.

Mafarao walianza kambi yao wiki moja iliyopita kwa ajili ya maandalizi hayo ya Afcon 2019, ambayo yanafanyika Misri, na kutarajia kuanza kutimua vumbi kuanzia Juni 21 hadi Julai 19 mwaka huu.

Hata hivyo, Salah katika kipindi chote hicho hakuwamo katika kambi ya timu hiyo hadi Jumatano baada ya kuhitaji mapumziko marefu baada ya kuiongoza Liverpool kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya jijini Madrid Juni Mosi.

Kwa mujibu wa taarifa, Salah alikuwamo katika mazoezi ya juzi, lakini hakutarajia kuwamo katika kikosi cha Misri ambacho kilitarajia juzi usiku kucheza na Tanzania (Taifa Stars), katika mchezo wa kujipima nguvu.

Hata hivyo, mchezaji huyo nyota ambaye ni miongoni mwa wafungaji walioongoza kwa ufungaji katika Ligi Kuu England, atakuwepo katika mchezo wa mwisho wa majaribio wakati Misri itakapocheza dhidi ya Guinea, Juni 16 kwenye Uwanja wa Borg El-Arab huko Alexandria.

Salah hatakuwa mchezaji pekee kurejea baada ya kutokuwapo katika mchezo wa Guinea, wakati mchezaji mwenzake wa Liverpool Naby Keita kutangaza kuwepo katika mchezo huo wa kirafiki.

Misri itaanza kampeni zake za kusaka taji hilo la Afrika kwa kucheza dhidi ya Zimbabwe Juni 21 katika mchezo wa Kundi A, kabla ya kukabiliana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Uganda Juni 26 na Juni 30.






# UNITED

## KUTOA OFA MPYA KWA DE GEA

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United ipo tayari kuongeza ofa zaidi kwa golikipa, David De Gea ili kumbakisha hapo kwenye uwanja wa Old Trafford baada ya Juni 2020, kwa mujibu wa ESPN FC.

De Gea, ameripotiwa kwamba anawaniwa na Klabu ya Paris Saint-Germain, na hivi karibuni alikataa ofa ya kuongeza mkataba wa miaka mitano na United ambapo angekuwa analipwa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki.

Makubaliano kwa ajili ya kusaini mkataba mpya yamekuwa yakiendelea kwa kipindi cha miezi 18 na yalionekana kusimama.

Na sasa imeripotiwa kwamba United wanajiandaa kutoa ofa mpya kwa De Gea ili kumlipa mamilioni ya fedha katika kipindi hiki cha majira ya joto.

Kama United watashindwa kumshawishi kuongeza mkataba mpya, maana yake ni kwamba, De Gea ataondoka akiwa huru kipindi kijacho cha majira ya joto.

Hata hivyo, United hawataki kumuuza De Gea kwa fedha kiasi chochote, kwani wanaimani kuwa wanaweza kumshawishi kusaini mkataba mpya.

De Gea kwa sasa anapokea kiasi cha pauni 240,000 kwa wiki, nusu ya mshahara wa mchezaji mwenzake, Alexis Sanchez anazolipwa.

# Unai apewa fedha kiduchu kusajili

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery ameripotiwa kupewa pauni milioni 40 kwenye bajeti yake ya usajili wa majira haya ya kipindi cha joto.

Bajeti hiyo inazua maswali mengi, ataweza kuunda kikosi cha aina gani kitakachokuwa na uwezo wa kushindania mataji msimu ujao na kubwa zaidi kurejea kwenye mchakamchaka wa Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kushindwa kufanya hivyo kwa misimu mitatu mfululizo.

Hata hivyo, kikosi cha Arsenal kinahitaji marekebisho kidogo tu, ambayo kama Kocha Emery atacheza karata zake sawa, basi ataunda timu itakayokuwa tishio kwenye Ligi Kuu England na pengine kukamatia tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2020/21.

Kikosi hicho cha Emirates huko Emirates, tayari kina mastaa wa maana kama Pierre-Emerick Aubameyang, Alexandre Lacazette, Mesut Ozil, Lucas Torreira, Matteo Guendouzi na wengineo, ambao atahitaji kuwabakiza kwenye timu ili aongeze wengine wachache tu kuifanya timu hiyo kuwa moto wa kuotea mbali.

Vita pekee ambayo inamkabili Emery ni kuhakikisha wakali hao wanabaki baada ya kudaiwa kusakwa na timu mbalimbali, ambapo Aubameyang anawindwa huko China, Lacazette Barcelona na Torreira huko Italia.



## HABARI MICHEZO



# TORONTO MABINGWA WAPYA NBA

**CALIFORNIA, Marekani**

TIMU ya mpira wa Kikapu ya Toronto Raptors imefanikiwa kuwa mabingwa wapya wa mchezo huo msimu huu nchini Marekani (NBA).

Hii ni mara ya kwanza kwa ligi hiyo maarufu zaidi duniani kwa mchezo wa kikapu bingwa wake kutoka nje ya Marekani.

Ikumbukwe kwamba, Ligi ya Soka la ile ya Kikapu hushirikisha nchi mbili za Marekani na Canada.

Raptors wameshika nafasi ya pili katika ligi hiyo kwa ushindi wa pointi 110-114 dhidi ya wapinzani wao Golden State Warriors, mchezo uliochezwa katika Uwanja wa Oracle Arena uliopo Oakland California.

Ushindi huo umeifanya Toronto Raptors kuibuka na ushindi wa jumla wa 4-2 dhidi ya Golden State Warriors na kuwa timu ya kwanza kutoka nchini Canada na nje ya Marekani kushinda ubingwa huo.

Sio hilo tu, Raptors pia haijawahi kufika fainali ya ligi hiyo tangu walipoingia kwa mara ya kwanza ligi hiyo mwaka 1995.

Kabla ya ushindi huo, timu za Canada hazijawahi kuwa na cha kujivunia kwani mara zote huishia katika mashindano madogo.

Taji la Raptors limemaliza nuksi ya timu za Canada kuendelea kuwa wasindikizaji, ambapo mara ya mwisho ilikuwa miaka 26 iliyopita (1993) pale Toronto Blue Jays iliposhinda taji ambalo hata hivyo si la NBA.

Katika ushindi huo, nyota Kyle Lowry na Mcameroon Pascal Siakam wote wawili walifunga pointi 26 kila mmoja wakiongoza kwa pointi ikiwamo ribaundi 10 za Siakam na asisti 10 pia za Lowry.

Upande wa Golden State Warriors, nyota Klay Thompson aliongoza kwa pointi zake 30 licha ya kushindwa kuendelea na mchezo dakika mbili za mwisho za robo ya kwanza katika kipindi cha pili akiumia mguu wa kushoto.

Kuumia kwa Klay ilikuwa pigo kubwa kwa Warriors kutokana na nyota huyo kutarajiwa kuamua mchezo wa leo baada ya kuwa na mchezo bora kabla ya kuumia baada ya nyota Steph Curry kudhibitiwa akifunga pointi 21 pekee.

Klay aliendeleza majanga kwa Warriors kufuatia kuumia kwake katika mchezo muhimu baada ya mchezo uliopita nyota mwingine Kevin Durant kuumia na kuipa pigo timu hiyo kujaribu kupindua matokeo ya 3-1.

Wachezaji wengine wa Warriors, Andre Iguodala alifunga pointi 22 wakati Draymond Green akitisha kwa kufunga pointi 11, ribaundi 18 na asisti 13.

Kwa matokeo hayo, Golden State Warriors wameshindwa kuendeleza ubabe waliokuwa nao ambapo walikuwa wametwaa taji hilo mara tatu ndani ya misimu minne iliyopita na walikuwa wanajaribu kutwaa ubingwa wa tatu mfululizo.

## RAIOLA ATUA PSG KUKAMILISHA USAJILI WA DE LIGT

**PARIS, Ufaransa**

WAKALA Mino Raiola amekutana na Mkurugenzi wa Klabu ya Paris Saint-Germain kwa ajili ya kukamilisha usajili wa beki wa timu ya Ajax, Matthijs de Ligt.

Raiola imeripotiwa kuwa amekutana na mkurugenzi huyo wa Paris Saint Germain kwa siri kubwa katika chumba cha hoteli kwa ajili ya kujadili uhamisho de Ligt.

PSG ineonekana iko mbioni kuipiku Barcelona kwenye mbio za kuwania kumsajili beki huyo mwenye umri wa miaka 19.

Ajax inaripotiwa kuwa wanataka pauni milioni 66.5 kwa ajili ya kutoa baraka kwa nahodha wao De Ligt kujiunga na PSG.

De Ligt ambaye ameichezwa Ajax zaidi ya michezo 100 hadi sasa mkataba wake unamalizika 2021 na msimu huu amekuwa gumzo kwa kuisaidia timu hiyo kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.



## Hazard atambulishwa rasmi Madrid

**MADRID, Hispania**

KIUNGO, Eden Hazard ametambulishwa rasmi kwa mashabiki wa Klabu ya Real Madrid baada ya kufuzu vipimo vya afya.

Real Madrid walimsajili Hazard kutoka Chelsea kwa ada inayotajwa kuwa ni pauni milioni 150 na alitambulishwa mbele ya mashabiki 50,000 katika Uwanja wa Santiago Bernabeu.

Real Madrid waliingia makubaliano ya kumsaini Hazard kwa mkataba wa miaka mitano kuwachezea miamba hao wa Hispania.

Mchezaji huyo wa Ubelgiji alifunga magoli 110 katika mechi 352 akiichezea Chelsea baada ya kujiunga kutoka Lille ya Ufaransa mwaka 2012 na kufunga magoli mawili waliposhinda kombe la ligi ya Europa akiwa na Chelsea.

"Kuondoka kwangu Chelsea ni uamuzi mkubwa na mgumu zaidi katika kipindi changu chote cha kucheza soka," alisema Hazardmara tu baada ya kukubali kusaini kuichezea Chelsea.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SARRI ARUHUSIWA KUTUA JUVENTUS

Ni baada ya Chelsea kukubali kulipwa fidia na mabingwa hao wa Italia...

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea imekubali mkataba unaomruhusu kocha wake, Maurizio Sarri kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Juventus.

Makubaliano hayo yamefikiwa Alhamisi jioni baada ya mazungumzo na maofisa wa ngazi ya juu na mkataba umekamilishwa jana Ijumaa.

Inafahamika kuwa gharama ya fidia ya ziada ya pauni milioni 5 imekubalika na pande husika.

Sarri aliwasili Chelsea kutoka Napoli Julai mwaka 2018 na kukiongoza kikosi cha Blues kufikia nafasi ya tatu katika Ligi Kuu ya England na kushinda kombe la Ligi ya Europa katika msimu wake mmoja wa uongozi wake.

Licha ya kusaini mkataba wa miaka mitatu Julai mwaka jana, atakuwa ni kocha wa tisa mwenye mkataba wa muda wote kuondoka chini ya mmiliki wa Chelsea, Roman Abramovich.

Kwa kipindi chote alichofanya kazi katika Stamford Bridge, Mtaliano huyo mwenye umri wa miaka 60, kumekuwa na tetesi za mara kwa mara kuhusu nafasi ya kazi yake, huku mashabiki wa Chelsea walielezea kutoridhishwa kwao na mbinu pamoja na namna timu inavyochaguliwa.

Moja ya matukio ambayo yalimshushia hadhi lilitokea Februari, ambapo mlinda mlango, Kepa Arrizabalaga alikaidi maagizo yake kwa kukataa kuondoka uwanjani alipoagizwa apumzike katika mchezo wa fainali ya Kombe la Carabao uliochezwa uwanja wa Wembley, muda mfupi kabla ya Chelsea kuchapwa kwa mkwaju wa penalti na Manchester City.

Lakini Sarri aliweza kushinda kombe lake la kwanza kabisa kama kocha kwa ushindi wa 4-1 dhidi ya Arsenal Mei katika fainali ya Ligi ya Europa.

Chelsea kwa sasa hawajaweza kumsajili mchezaji yeyote baada ya kupigwa marufuku kwa misimu miwili ya uhamisho na Shirikisho la Soka la Kimataifa, Fifa, uamuzi ambao wameupinga na kukata rufani dhidi yake katika mahakama ya utatuzi wa mizozo ya michezo.

Mchezaji wao nyota, Eden Hazard amejiunga na Real Madrid kwa gharama ambayo inatajwa kuwa ni pauni milioni 150.

Hii inamaanisha kuwa mchezaji mpya atakayewasili kwenye klabu hiyo huenda akawa ni mshambuliaji wa Marekani, Christian Pulisic, aliyesaini mkataba wa pauni milioni 58 kutoka Borussia Dortmund Januari mwaka huu.

Juventus hawana kocha baada ya Massimiliano Allegri kuondoka mwishoni mwa msimu uliopita, baada ya kushinda ligi katika kila moja ya misimu mitano tangu achukue uongozi mwaka 2014.

Baada ya kusifiwa kwa mbinu zake katika Napoli, alitaka kuanzisha 'mpira wa Sarri ' kwa wachezaji wake wapya wakati Chelsea ilipoanzisha kampeni yake ya Ligi Kuu kwa kucheza mechi 12 bila kufungwa.

## KWA UFUPI

**JUVE WAMFUATA POGBA**

MKURUGENZI wa Michezo wa Juventus, Fabio Paratici, anatarajia kusajili kwenda London katika ofisi za Manchester United ili kufanya mazungumzo ya ana kwa ana kwa ajili ya kufanikisha kumhamisha kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba, 26. ***(Sky Sports Italy, via Sky Sports)***

**LUKAKU, INTER SAFI**

STRAIKA wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku, tayari amefikia makubaliano binafsi na Inter Milan ambayo yatamfanya nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 kulipwa bonasi ya pauni milioni 6.6 hadi mwisho wa mkataba wake ambapo ni mwaka 2024. ***(Gazzetta dello Sport, via Metro)***

**CITY YAJIULIZA KWA MAGUIRE**

MABOSI wa Manchester City wameamua kusitisha mchakato wa kumsajili beki wa kati wa Leicester na Timu ya Taifa ya England, Harry Maguire (26) ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 90, kwa kuyaweka kiporo majadiliano juu ya uhamisho huo. ***(Mail)***

**FERNANDES AKARIBIA UTD**

MANCHESTER United inaongoza katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa Timu ya Taifa ya Ureno, Bruno Fernandes ambaye anaichezea Sporting Lisbon, klabu nyingine zinazomwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 ni Liverpool na Manchester City. ***(Radio Rossonera, via Sun)***

**KOSCIELNY ATAKIWA DORTMUND**

BORUSSIA Dortmund ya Ujerumani inamfuatilia kwa karibu beki Mfaransa wa Arsenal, Laurent Koscielny, mwenye umri wa miaka 33 ambaye anaweza kuruhusiwa kuondoka klabuni hapo katika kipindi cha majira ya joto. ***(Mail)***

**WAN-BISSAKA KITAELEWEKA**

BEKI wa kulia wa Crystal Palace ambaye ni raia wa England, Aaron Wan-Bissaka (21), anapewa nafasi kubwa ya kujiunga na Manchester United katika kipindi cha majira ya joto. Thamani ya beki huyo wa Palace imetajwa kuwa ni pauni milioni 70. ***(Sky Sports)***

**SPURS KUVUNJA REKODI**

KLABU ya Tottenham inajiandaa kuvunja rekodi ya usajili mara mbili kwa kumnasa kiungo mchezeshaji wa Real Betis na Timu ya Taifa ya Argentina, Giovani lo Celso (23) pamoja na kiungo wa Ufaransa na Lyon, Tanguy Ndombele ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Mirror)***

**VALVERDE AMRUHUSU RAKITIC**

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde atamruhusu kiungo wa Timu ya Taifa ya Croatia, Ivan Rakitic (31), kuondoka klabuni hapo kama watapokea ofa inayolingana na thamani ya mchezaji huyo. ***(Cadena SER - in Spanish)***

**SCHUBERT KUTUA ARSENAL**

ARSENAL iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mchakato wa kumsajili golikipa Mjerumani Markus Schubert ambaye ana umri wa miaka 21, kutoka klabu ya Dynamo Dresden. ***(Independent)***

**NERES AGOMBEWA ULAYA**

EVERTON na Paris St-Germain zote zimetajwa kumwania mshambuliaji wa Ajax Mbrazili David Neres ambaye ana umri wa miaka 22, katika kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Esporte - in Spanish)***

**PSG: RABIOT HAONDOKI**

KIUNGO wa PSG na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Adrien Rabiot (24), ataendelea kubakia kwa mabingwa hao wa Ligue 1 licha ya kuondoka klabuni hapo katika mzunguko wa pili wa msimu uliomalizika. ***(ESPN)***

**FRASER AIKATAA ARSENAL**

WINGA wa Bournemouth kutoka Scotland, Ryan Fraser, ambaye anatakiwa na Arsenal, amebainisha kuwa ataendelea kubakia katika klabu hiyo maarufu kwa jina la Cherries kwa mwaka mmoja zaidi. ***(Mirror)***

**MEUNIER AIKUBALI PSG**

BEKI wa kulia wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Thomas Meunier, ambaye anahusishwa na tetesi za kujiunga na Arsenal, amesema kuwa anataka kubakia katika klabu yake hiyo ya PSG. ***(Express)***

## HABARI MICHEZO

# NDUGAI KUONGOZA WABUNGE KUWASHANGILIA STARS AFCON

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, anatarajiwa kuongoza wabunge 83 kwenda kuishangilia Timu ya Taifa (Taifa Stars) katika Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) zitakazofanyika nchini Misri kuanzia Juni 21 hadi Julai 19 mwaka huu.

Stars iko Kundi C na itaanza mechi yake ya kwanza Juni 23 mwaka huu dhidi ya Senegal wakati siku ya ufunguzi Misri itaikaribisha Zimbabwe.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mwenyekiti wa Timu ya Bunge, William Ngeleja, alisema wabunge 83 wamejiorodhesha ili kushuhudia fainali hizo.

Ngeleja alifafanua kuwa kutokana na vikao vya Bunge kuendelea, wabunge hao wamegawanywa kwenye makundi mawili ambapo kundi la kwanza litaondoka Juni, 20 mwaka huu, kutokea jijini hapa kwenda kushiriki ufunguzi na mechi itakayochezwa Juni, 23 mwaka huu.

"Hili kundi litarejea Dodoma Juni 24, mwaka huu ili kuwahi zoezi la kuhitimisha mjadala wa bajeti Juni 25, mwaka huu na mara baada ya kumalizika, kundi la pili litaondoka Juni 26, mwaka huu na litarejea nchini Julai 2, mwaka huu na litaishia Dar es salaam kwa kuwa Bunge litakuwa limeahirishwa," alisema.

Aidha, aliipongeza Taifa Stars katika mechi ya kirafiki iliyochezwa juzi dhidi ya Misri ambapo Misri (Mafarao) waliibuka na ushindi wa bao 1-0.

"Tunaamini mechi hii imejenga msingi mzuri wa wao kushiriki fainali hizi,"alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa Spika ambaye ni Mratibu wa safari hiyo, Saidi Yakubu, alisema Spika Ndugai ataongoza kundi la kwanza la wabunge litakaloshuhudia ufunguzi na mechi ya Taifa Stars dhidi ya Senegal.

Naye Kocha wa Timu ya Bunge, Venance Mwamoto, alisema wanaiombea timu hiyo ifanye vizuri lakini safari yao pia itatangaza vivutio vya utalii nchini na upatikanaji wa korosho.




Kocha wa Gwambina FC, Fulgence Novatus akionyesha mazingira ya uwanja mpya wa timu hiyo uliopo katika Wilaya ya Misungwi jijini Mwanza ambao utafunguliwa rasmi Juni 21, mwaka huu kwa mechi ya kirafiki dhidi ya mabingwa wa Bara, Simba. **PICHA: ROSE JACOB**

# Polisi Tanzania wamtangaza Matola

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa "Maafande" wa Polisi Tanzania itakayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao imemtangaza Selemani Matola, kutoka Lipuli FC kuwa kocha wake mpya.

Mbali na Polisi Tanzania, timu nyingine iliyopanda daraja ni pamoja na Namungo FC ya mkoani Lindi.

Matola alikuwa pia anahusishwa na mipango ya kujiunga na KMC FC ya jijini Dar es Salaam baada ya aliyekuwa kocha wake, Etienne Ndayiragije, kuhamia Azam FC.

Akizungumza jana jijini, Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi, alisema jana kuwa Matola amesaini mkataba wa mwaka mmoja na uamuzi wa kumwajiri kocha huyo umetokana na kufahamu uwezo na uzoefu wake.

Munisi alisema kuwa wanaamini chini ya Matola, kikosi chao kitaimarika na kitakuwa moja ya timu zitakazotoa ushindani katika kila mechi watakayocheza.

"Tunapenda kumtangaza rasmi, Selemani Matola, ameingia katika familia ya Polisi Tanzania, tutaahidi kumpa ushirikiano ili aweze kufanya vema majukumu yake," alisema Munisi.

Aliongeza kuwa timu hiyo ambayo ilikuwa inatumia Uwanja wa Chuo cha Polisi Moshi ilipokuwa Ligi Daraja la Kwanza, sasa itahamia mkoani Dodoma.

Matola aliliambia Nipashe kuwa anashukuru kupata nafasi ya kujiunga na Polisi Tanzania, na kwa pamoja amejiandaa kuifanya timu hiyo iwe imara na iweze kupambana katika mashindano yote watakayoshiriki.

"Nashukuru kwa kupata heshima hii, nimekubali kujiunga na timu hii na ninaamini watapata kile wanachokitarajia, kazi ya mpira inaonekana hadharani," Matola, kiungo wa zamani wa Simba Supersport ya Afrika Kusini alisema.

Msimu uliomalizika, Matola alimaliza katika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kucheza fainali ya Kombe la FA.

## Ruvuma Queens, TSC mambo safi

**Na Mwandishi Wetu, KIBAHA**

TIMU ya Ruvuma Queens kutoka mkoani Ruvuma imeendelea kujiweka katika mazingira mazuri ya kupanda daraja baada ya kuifunga Sayari Woman FC mabao 10-2 katika mechi ya Ligi Daraja la Kwanza iliyochezwa juzi mjini hapa.

Kwa matokeo hayo, Ruvuma Queens imefikisha pointi sita na kuongoza katika Kundi B.

Ruvuma Queens sasa watasubiri kucheza mechi moja ya fainali ambayo itatoa bingwa wa ligi hiyo ambayo itapandisha klabu mbili kucheza Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu ujao.

TSC Queens ya jijini Mwanza nayo imejiweka katika nafasi nzuri baada ya kupata ushindi wa mabao 3-1 katika mchezo mwingine uliochezwa kwenye Uwanja wa Filbert Bahi.

Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Wanawake Tanzania (TWFA), Amina Karuma, alisema kuwa amefurahishwa kuona wachezaji wapya wakionyesha vipaji katika ligi hiyo.

Karuma alisema kuwa ligi hiyo inaendelea kutoa nafasi kwa makocha wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) kupata wachezaji wengine watakaoimarisha kikosi hicho.

## M-BET kuwapeleka washangiliaji Misri

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha Timu ya Taifa (Taifa Stars) inapata nguvu kwa kushangiliwa na wazawa, kampuni ya michezo ya kubahatisha ya M-BET imesema itapeleka mashabiki kuhudhuria Fainali ya Mataifa ya Afrika (Afcon) zinazotarajiwa kufanyika kuanzia Juni 21 mpaka Julai 19 mwaka huu, nchini Misri.

Hayo yalisemwa na Meneja Masoko wa M-BET Tanzania, Allen Mushi, wakati wa kumzawadia, Samwel Jonas mkazi wa Karatu, Mkoa wa Manyara, aliyeshinda kitita cha Sh. milioni 125. 5 baada ya kubashiri kwa usahihi michezo 12 ya droo ya Perfect 12.

Mushi alisema kuwa mashabiki wa soka wanatakiwa kubashiri mechi 10 na kuingia katika droo maalum ambayo itatoa washindi watakaokwenda Misri kushuhudia mchezo kati ya Taifa Stars dhidi ya Kenya ambayo utakaochezwa Juni 27, mwaka huu.

Alisema kuwa washindi hao pia watapata fursa ya kuona mechi ya mwisho ya hatua ya makundi ambayo itakuwa ni kati ya Stars dhidi ya Algeria iliyopangwa kufanyika Julai Mosi na kutembelea vivutio vya kitalii nchini humo.

Mbali ya mashabiki wa soka kwenda Misri, M-Bet pia itawazawadia Watanzania zawadi ya jezi kwa mashabiki wa soka watakaoweza kucheza tiketi tatu katika michezo yoyote.

# Michezo

Jumamosi Juni 15, 2019

Nipashe




## Sarri aruhusiwa kutua Juventus

HABARI UK 30



Nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta (katikati), akijaribu kuondoka na mpira katika mechi ya kirafiki dhidi ya Misri iliyochezwa juzi usiku mjini Alexabdria. Stars ililala bao 1-0. **PICHA: TFF**

# KAKOLANYA RASMI ASAJILIWA SIMBA

●●●Ni baada ya kuitingisha Yanga ambayo leo inaendesha harambee ya "Kubwa Kuliko"...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wakiendelea kuimarisha kikosi chao kwa kunasa saini ya kipa, Beno Kakolanya, watani zao Yanga leo wanatarajia kufanya harambee ya kihistoria ili kukusanya fedha kwa lengo la kusajili wachezaji watakaowatumia kwenye msimu ujao.

Mabingwa hao wa Bara, jana mchana walitangaza kumsajili Kakolanya, ambaye alikuwa mchezaji huru kwa kumpa mkataba wa miaka miwili.

Kakolanya alitangazwa kuwa huru baada ya Yanga kushindwa kumlipa malimbikizo ya mshahara wake na hivyo kuamua kukaa pembeni.

Kipa huyo atatakiwa kupambana kuwania namba dhidi ya mlinda mlango chaguo la kwanza la Wekundu wa Msimbazi, Aishi Manula na Deogratius Munishi "Dida" ambaye mpaka sasa hatima yake kikosini hapo haijajulikana.

**"Ni Beno Kakolanya. Hakuna ubishi kuwa huyu ni moja ya makipa wenye uwezo mkubwa nchini na tunaamini akishirikiana na wenzake katika kikosi chetu, watatuwezesha kuongeza ukubwa wa timu na kutupatia mataji zaidi msimu ujao, tumemalizana naye," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori.**

Kiongozi huyo alisema kuwa Simba imejipanga kuimarisha safu zote katika kikosi chake kwa sababu inataka kupata mafanikio zaidi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Taarifa zaidi kutoka Simba zinasema kuwa tayari wamefanikiwa kumrejesha beki, Miraji Athumani ambaye msimu uliopita alikuwa katika kikosi cha Lipuli FC ya mkoani Iringa.

**MAJALIWA, KIKWETE NDANI**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuongoza harambee ya klabu ya Yanga iliyopewa jina la "Kubwa Kuliko" itakayofanyika leo kwenye Ukumbi wa Diamond Jubilee jijini kuanzia saa 4:00 asubuhi.

Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya harambee hiyo, David Ruhago, alisema jana kuwa maandalizi yamekamilika na alimtaja Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete naye anatarajiwa kuhudhuria akiwa ni mgeni maalumu.

"Hii ni fursa adimu kwa kila Mwanajangwani kupata nafasi ya kujumuika na Wanayanga wengine katika harambee hii yenye lengo la kuirudisha Yanga mahali pake," alisema Ruhago. Alisema kuwa wanaamini baada ya harambee hiyo, Yanga itarejea katika hadhi na ushindani kwa kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano yote watakayoshiriki.

## Samatta afunguka Misri imewajenga

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Emmanuel Amunike, amesema kuwa mchezo wa kirafiki dhidi ya Misri (Mafarao) ulikuwa ni muhimu kwa kikosi chake, kwa sababu kiufundi bado kinaendelea kuimarika, nahodha wa timu hiyo, Mbwana Samatta, amesema mechi hiyo imesaidia kuwajenga.

Taifa Stars ambayo ilimaliza dakika 45 za kipindi cha kwanza bila ya kuruhusu goli, ilipoteza mchezo huo wa kirafiki uliochezwa juzi usiku kwenye Uwanja wa Borg El Arab mjini Alexandria kwa kufungwa bao 1-0. Akizungumza na gazeti hili jana, Amunike, alisema kuwa mchezo huo umemsaidia kufahamu makosa ya wachezaji wake na hivyo atayafanyia kazi kabla ya kuanza kwa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika hapo wiki ijayo.

Amunike alisema kwamba kujipima na timu kubwa ni jambo jema kwa sababu kwa upande wake anapata faida ya kujitathmini na kurekebisha pale penye udhaifu katika kikosi chake ambacho kina wachezaji wengi wanaocheza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara tofauti na ilivyokuwa kwa wapinzani wao.

"Ilikuwa ni nafasi muhimu sana kucheza na Misri, ni timu kubwa sana barani Afrika ambayo ina wachezaji wanaocheza Ulaya na wenye uzoefu, imenisaidia kujua ninapotakiwa kurekebisha, katika mpira hapa tumefanikiwa zaidi, tutakuwa imara kuelekea michuano hii ya Afrika," alisema Amunike.

Naye nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, alisema kuwa amefurahi kujipima na timu kubwa na hapo ndio wakati mzuri wa benchi la ufundi kufahamu upungufu wa kikosi na kujipanga kuufanyia kazi.

"Wana timu nzuri, wako imara, ni moja ya timu bora barani Afrika, ndio maana ya kucheza mechi za kirafiki, tutajua wapi tumekosea ili tuweze kujirekebisha, tunafahamu tutacheza mechi ngumu katika makundi na mechi hii itatusaidia kujitambua na kurekebisha pale tulipokosea," alisema Samatta.

Hata hivyo, katika mchezo huo wa kirafiki, wenyeji Misri hawakuwachezesha nyota wake kadhaa akiwamo mshambuliaji wa Liverpool ya England, Mohammed Salah ambaye alikuwa benchi na kuonekana kufurahi wakati mechi hiyo ikiendelea.

Stars itashuka tena dimbani kesho katika mchezo mwingine wa kirafiki dhidi ya wenzao wa Zimbabwe katika mwendelezo wa kukiimarisha kikosi hicho.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >